# TAARIFA YA TATHMINI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2020

Tume ya Taifa ya Uchaguzi,

Uchaguzi House,

Eneo la Uwekezaji Njedengwa,

Kitalu D, Kiwanja Na. 4,

S.L.P. 358,

DODOMA.

© Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2021

ISBN 978 - 9976 - 9957 - 9 - 4

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili au kutoa kitabu hiki kwa njia yoyote ile bila idhini kwa maandishi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

# YALIYOMO

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... iv
**ORODHA YA CHATI** .......... v
**ORODHA YA MICHORO NA VIAMBATISHO** .......... vi
**VIFUPISHO VYA MANENO** .......... vii
**SHUKRANI** .......... viii
**DIBAJI** .......... ix
**MUHTASARI WA TAARIFA** .......... xi
**SURA YA KWANZA** .......... 1
**UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi .......... 1
1.1.1 Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi .......... 1
1.1.2 Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi .......... 2
1.2 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania .......... 3
**SURA YA PILI** .......... 5
**TATHMINI YA UCHAGUZI MKUU** .......... 5
2.1. Utangulizi .......... 5
2.2 Tathmini ya Uchaguzi Mkuu .......... 6
2.3 Msingi wa Tathmini .......... 6
2.3.1 Kukamilisha Mzunguko wa Uchaguzi .......... 7
2.3.2 Mwongozo wa Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Mwaka 2014 .......... 7
2.3.3 Mpango Mkakati wa Tume wa Mwaka 2016/17 - 2020/21 .......... 7
2.4 Malengo ya Kufanya Tathmini .......... 7
2.4.1 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura .......... 8
2.4.2 Ushirikishwaji wa Wadau katika Mchakato wa Uchaguzi .......... 8
2.4.3 Kampeni za Uchaguzi .......... 8
2.4.4 Ufanisi wa Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume .......... 9
2.4.5 Kupima Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura katika Mchakato wa Uchaguzi .......... 9
2.4.6 Mrejesho wa Jinsi Zoezi la Kupiga Kura Lilivyofanyika .......... 10
2.4.7 Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo wa Wapiga Kura .......... 10
2.4.8 Uwepo wa Kura Zilizokataliwa .......... 11
**SURA YA TATU** .......... 13

**MBINU ZILIZOTUMIKA KUFANYA TATHMINI** .......... 13
3.1 Utangulizi .......... 13
3.2 Wigo na Maeneo ya Tathmini .......... 13
3.3 Vigezo Vilivyotumika Kuchagua Maeneo ya Tathmini .......... 14
3.3.1 Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo .......... 15
3.3.2 Maeneo Yenye Mwitikio wa Wastani .......... 16
3.3.3 Maeneo Yenye Mwitikio Mkubwa .......... 16
3.3.4 Maeneo Yenye Kura nyingi Zilizokataliwa .......... 17
3.4 Njia Zilizotumika Kukusanya Takwimu .......... 18
3.4.1 Mahojiano ya Ana kwa Ana .......... 18
3.4.2 Majadiliano na Makundi Maalum .......... 21
3.4.3 Mikutano na Watendaji wa Uchaguzi .......... 23
3.4.4 Mapitio ya Nyaraka .......... 25
3.5 Sampuli ya Waliohojiwa .......... 25
3.6 Uchambuzi wa Takwimu .......... 26
**SURA YA NNE** .......... 27
**MATOKEO YA TATHMINI** .......... 27
4.1 Utangulizi .......... 27
4.2 Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume .......... 27
4.3 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura .......... 30
4.3.1 Ufanisi wa Mashine za Kuandikishia Wapiga Kura kwa Kutumia Alama za Kibaiolojia - BVR .......... 31
4.3.2 Upatikanaji wa Kadi ya Mpiga Kura .......... 32
4.3.3 Muda wa Kujiandikisha .......... 32
4.3.4 Uhakiki wa Taarifa wakati wa Uwekaji wazi wa Daftari la Awali .......... 33
4.3.5 Njia Zilizotumika Kuhakiki Taarifa za Mpiga Kura .......... 34
4.3.6 Changamoto Wakati wa Uboreshaji .......... 35
4.3.7 Maoni Kuhusu Mchakato wa Uboreshaji .......... 36
4.4 Elimu ya Mpiga Kura .......... 37
4.4.1 Muda wa Kutoa Elimu ya Mpiga Kura .......... 38
4.4.2 Vifaa vya Elimu ya Mpiga Kura .......... 38
4.4.3 Njia Zilizotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura .......... 38
4.4.4 Uelewa wa Haki ya Kupiga Kura .......... 40

4.4.5 Mapendekezo ya Kuboresha Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura ............... 41
4.5 Wapiga Kura Wenye Mahitaji Maalum ............... 42
4.6 Ushirikishwaji wa Wadau wa Uchaguzi ............... 43
4.7 Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura ............... 45
4.8 Kampeni za Uchaguzi ............... 46
4.9 Vifaa vya Uchaguzi ............... 48
4.10 Mawakala wa Vyama vya Siasa ............... 50
4.10.1 Kiapo cha Mawakala ............... 51
4.10.2 Mawakala Kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume ............... 51
4.11 Vituo vya Kupigia Kura ............... 53
4.11.1 Kufikika kwa Vituo vya Kupigia Kura ............... 54
4.11.2 Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura ............... 55
4.12 Kupiga na Kuhesabu Kura ............... 56
4.12.1 Muda wa Kufungua Vituo vya Kupigia Kura ............... 57
4.12.2 Jinsi ya Wapiga Kura ............... 58
4.12.3 Umri wa Wapiga Kura Waliojitokeza Kupiga Kura ............... 59
4.12.4 Changamoto Wakati wa Kupiga na Kuhesabu Kura ............... 60
4.12.5 Kura Zilizokataliwa ............... 61
4.13 Kuhesabu, Kujumlisha na Kutangaza Matokeo ............... 62
4.13.1. Matokeo ya Tathmini Kuhesabu, Kujumlisha na Kutangaza Matokeo . 63
4.14 Mwitikio wa Wapiga Kura ............... 65
4.15 Taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi, Taasisi na Asasi zilizotoa Elimu ya Mpiga Kura ............... 68
4.15.1 Mafanikio ............... 69
4.15.2 Changamoto ............... 70
4.15.3 Maoni na Mapendekezo ............... 70
**SURA YA TANO** ............... 74
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ............... 74
5.1 Hitimisho ............... 74
5.2 Mapendekezo ............... 76

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Mwitiko wa Wapiga Kura katika Chaguzi Mbalimbali ........ 11
Jedwali Na. 2: Kura Zilizokataliwa katika Chaguzi Mbalimbali ........ 12
Jedwali Na. 3: Mgawanyo wa Mwitikio wa Wapiga Kura ........ 15
Jedwali Na. 4: Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo ........ 15
Jedwali Na. 5: Maeneo Yenye Mwitikio wa Wastani ........ 16
Jedwali Na. 6: Maeneo Yenye Mwitikio Mkubwa ........ 17
Jedwali Na. 7: Maeneo Yenye Kura nyingi Zilizokataliwa ........ 17
Jedwali Na. 8: Aina ya Makundi Maalum Yaliyofanya Majadiliano ........ 22
Jedwali Na. 9: Sampuli ya Waliohojiwa kwa Jinsi ........ 25
Jedwali Na. 10: Mgawanyo wa Waliohojiwa kwa Umri ........ 26
Jedwali Na. 11: Ufanisi wa Njia Zilizotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura ........ 39

# ORODHA YA CHATI


Chati Na. 1: Kueleweka kwa Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume ........ 29
Chati Na. 2: Muda wa Kujiandikisha ........ 33
Chati Na. 3: Uelewa wa Haki ya Kupiga Kura ........ 40
Chati Na. 4: Wapiga Kura Wenye Mahitaji Maalum na Makundi Maalum katika Jamii Kupewa Kipaumbele Siku ya Kupiga Kura ........ 43
Chati Na. 5: Mawakala Kuzingatia au Kutozingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume ........ 52
Chati Na. 6: Kufikika kwa Vituo vya Kupigia Kura ........ 54
Chati Na. 7: Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura ........ 56
Chati Na. 8: Muda wa Kufungua Vituo vya Kupigia Kura ........ 57
Chati Na. 9: Makundi kwa Umri wa Wapiga Kura Waliojitokeza Kupiga Kura ... 59
Chati Na. 10: Changamoto Wakati wa Kupiga na Kuhesabu Kura ........ 60
Chati Na. 11: Utumaji wa Matokeo ya Kiti cha Rais kwenda Tume ........ 64
Chati Na. 12: Mwitikio wa Wapiga Kura kwa Chaguzi Kuu Sita ........ 65

# ORODHA YA MICHORO NA VIAMBATISHO

Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi ....... 4
Mchoro Na. 2: Majimbo Yaliyofanyiwa Tathmini ....... 18
Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Mikoa na Halmashauri/Wilaya zilizofanyiwa Tathmini ....... 78
Kiambatisho Na. 2: Mpango wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ....... 81

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BVR | Biometric Voters' Registration |
| CC | City Council |
| CCK | Chama cha Kijamii |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CUF | Civic United Front |
| DC | District Council |
| DP | Democratic Party |
| EISA | Electoral Institute for Sustainable Democracy in Africa |
| MC | Municipal Council |
| Na. | Namba |
| NCCR-Mageuzi | National Convention for Construction and Reform-Mageuzi |
| NEC | National Electoral Commission |
| SMS | Short Message Services |
| SPSS | Statistical Package for the Social Sciences |
| TC | Town Council |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UMD | Union for Multiparty Democracy |

## SHUKRANI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekamilisha tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tathmini imefanyika ili kupata taswira ya jinsi uchaguzi ulivyoendeshwa na kupata maoni yatakayosaidia kuboresha chaguzi zijazo. Aidha, Tume isingeweza kukamilisha zoezi hili pasipo ushirikiano wa wadau mbalimbali wa uchaguzi ambao walishiriki katika kutoa maoni na mapendekezo wakati wa majadiliano na mahojiano yaliyofanyika ili kukusanya taarifa.

Tume inatoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano uliowezesha kufanyika na kukamilika kwa tathmini hii.

Vilevile, Tume inawashukuru wapiga kura, vyama vya siasa, makundi maalum, wananchi na wadau wengine wote ambao kwa njia mbalimbali walichangia kufanikisha zoezi hili.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaamini kuwa taarifa hii ya tathmini itatumiwa na wadau wa uchaguzi ikiwa ni nyenzo muhimu katika kufanya maboresho na maandalizi ya chaguzi zijazo.



Jaji (R) (Mst.) Semistocles S. Kaijage

**MWENYEKITI**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi

## DIBAJI

Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 uliendeshwa kwa mafanikio. Matokeo hayo yametokana na ushirikiano ambao Tume ilipata kutoka kwa wadau wa uchaguzi ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vyama vya siasa, watazamaji wa uchaguzi, vyombo vya habari, wapiga kura, taasisi na asasi za kiraia pamoja na wadau wengine.

Aidha, mafanikio hayo yamechangiwa zaidi na jinsi watendaji na wadau wa uchaguzi walivyotekeleza wajibu wao kwa kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume pamoja na matumizi ya mifumo ya kieletroniki ya uchaguzi. Hali hii iliwezesha kuwa na uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika.

Taarifa hii imeainisha maoni na mapendekezo ya wadau walioshiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Maoni yaliyotolewa yameangazia utendaji wa Tume katika kuratibu, kusimamia na kutekeleza shughuli za uchaguzi katika hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, maandalizi ya vifaa vya uchaguzi, uteuzi wa watendaji wa uchaguzi, uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha na kutangaza matokeo. Vilevile, tathmini imeainisha changamoto zilizobainishwa katika kila hatua na mapendekezo yaliyotolewa na wadau ya kuboresha chaguzi zijazo.

Tathmini hii inakusudiwa kutoa mrejesho kwa wadau wa uchaguzi juu ya namna ambavyo Tume imetekeleza jukumu lake la kikatiba na

kisheria katika kusimamia na kuratibu uendeshaji wa shughuli za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tume inatarajia kuwa, matokeo yaliyopatikana yatatumika kuboresha utekelezaji wa shughuli za Tume ili kuzifanya chaguzi zijazo kuwa bora zaidi.

# MUHTASARI WA TAARIFA

Taarifa hii inahusu tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 iliyofanyika kuanzia Novemba, 2020 hadi Disemba, 2020. Lengo lilikuwa kupata mrejesho kutoka kwa wadau jinsi Tume ilivyotekeleza majukumu yake wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Taarifa ya tathmini imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi ambayo inaelezea mfumo wa siasa Tanzania, majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na muundo wa Tume. Sura ya pili inaelezea misingi, malengo na matarajio ya tathmini. Sura ya tatu inaelezea wigo na vigezo vilivyotumika katika kuchagua maeneo ya kufanyia tathmini, njia zilizotumika kukusanya takwimu na uchakataji wa takwimu. Sura ya nne inaelezea matokeo ya tathmini na sura ya tano ni hitimisho na mapendekezo.

Tathmini imefanyika katika mikoa 24 kati ya hiyo, mikoa 22 ni ya Tanzania Bara na mikoa miwili (2) ni ya Tanzania Zanzibar. Katika mikoa hiyo, tathmini ilifanyika katika majimbo 48 ambapo majimbo 44 yalikuwa ya Tanzania Bara na majimbo manne (4) yalikuwa ya Tanzania Zanzibar. Kwa ujumla, tathmini ilihusisha jumla ya walengwa 1,874 miongoni mwao wakiwemo waratibu wa uchaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata, maafisa ugavi, maafisa uchaguzi, viongozi wa vyama vya siasa, wapiga kura, makundi ya wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. Pia, ilihusisha kupitia taarifa za watazamaji wa uchaguzi wa ndani na wa kimataifa pamoja na asasi au taasisi zilizopata vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura.

Vigezo vilivyotumika kuchagua maeneo ya kufanya tathmini vilizingatia mwitikio wa wapiga kura, idadi ya kura zilizokataliwa na uwakilishi wa kanda za uchaguzi na idadi ya wapiga kura. Ukusanyaji wa takwimu ulifanyika kwa njia ya madodoso, mahojiano ya ana kwa ana, mikutano na watendaji wa uchaguzi, majadiliano na makundi ya wazee, walemavu, wanawake na vijana.

Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa, Tume imetekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria kwa ufanisi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Hii inadhihirishwa na uwepo wa kesi chache zilizofunguliwa kupinga matokeo au mwenendo wa uchaguzi ambapo kwa ujumla kesi 15 zilifunguliwa. Kwa upande wa Ubunge kesi nne (4) zilifunguliwa na kwa upande wa madiwani zilifunguliwa kesi 11. Idadi hii ya kesi ni ndogo ikilinganishwa na kesi 246 za uchaguzi zilizofunguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ambapo kesi 52 zilikuwa za Ubunge na kesi 194 zilikuwa za Udiwani.

Vilevile, matokeo yanaonesha kuwa Tume ilifanya vizuri katika kuwashirikisha wadau wa uchaguzi, kuratibu kampeni za uchaguzi, kutoa elimu ya mpiga kura, kusimamia mchakato wa kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangaza matokeo. Pamoja na mafanikio yaliyoonekana, matokeo ya tathmini yamebainisha kuwepo kwa changamoto kadhaa katika baadhi ya maeneo kama utoaji elimu ya mpiga kura, uapishaji wa mawakala, kampeni za uchaguzi na mwitikio wa wapiga kura siku ya uchaguzi.

Tathmini imeainisha mapendekezo ya wadau na jinsi ya kuboresha utekelezaji wa shughuli za Tume katika baadhi ya maeneo kwa

chaguzi zijazo. Mapendekezo yanalenga kuboresha sheria za uchaguzi, utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa kuifanya iwe endelevu na kuongeza mwitikio wa wapiga kura katika chaguzi zijazo.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Tume ilianzishwa tarehe 13 Januari, 1993 kwa kuzingatia masharti ya ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kwa mujibu wa ibara ya 74(7) ya Katiba, Tume ni idara huru inayojitegemea na inafanya maamuzi rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao.

### 1.1.1 Muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa kuzingatia ibara ya 74(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume inaundwa na Wajumbe saba. Wajumbe hao ni Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ambao wanapaswa kuwa na sifa ya Jaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au mtu mwenye sifa ya kuwa Wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka 15. Katika uteuzi wao, Rais atazingatia kuwa endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano.

Mjumbe mwingine atateuliwa kutoka miongoni mwa wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society - TLS). Wajumbe wanne watatakiwa wawe na uzoefu wa kutosha wa kuendesha au kusimamia uchaguzi wa Wabunge au sifa nyingine kama ambavyo Rais wa Jamhuri ya Muungano atakavyoona inafaa kwa utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Ibara ya 74 (7) ya Katiba ikisomwa pamoja na kifungu cha 4(4) na 6 vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Mkurugenzi wa Uchaguzi ndiye Katibu na Mtendaji Mkuu wa Tume. Tume inazo idara sita, ofisi ya Zanzibar na vitengo vitatu vinavyoongozwa na Wakurugenzi na Wakuu wa vitengo. Idara na vitengo hivyo ni vifuatavyo: -

(i) Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu;
(ii) Idara ya Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini;
(iii) Idara ya Usimamizi wa Ununuzi na Lojistiki;
(iv) Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi;
(v) Idara ya Uandikishaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na TEHAMA;
(vi) Idara ya Habari na Elimu ya Mpiga Kura;
(vii) Ofisi ya Zanzibar;
(viii) Kitengo cha Uhasibu na Fedha;
(ix) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani; na
(x) Kitengo cha Huduma za Sheria.

### 1.1.2 Majukumu ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 74(6) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, majukumu ya Tume ni haya yafuatayo:-

(i) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;

(ii) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge;

(iii) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;

(iv) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa uchaguzi wa madiwani;

(v) kutoa Elimu ya mpiga kura kwa nchi nzima pamoja na kuratibu, kusimamia taasisi na watu wanaotoa elimu hiyo;

(vi) kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalum; na


(vii) kuteua na kuwatangaza Madiwani Wanawake wa Viti Maalum.

## 1.2 Mzunguko wa Uchaguzi Tanzania

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inasimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Uchaguzi huo hufanyika kila baada ya kipindi cha miaka mitano.

Jukumu hilo hutekelezwa kwa mujibu wa ibara ya 65 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 12 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Tume hufuata mzunguko wa uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu. Awamu hizo ni shughuli kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Shughuli katika awamu hizo zimeoneshwa kwenye Mchoro Na. 1.

## Mchoro Na. 1: Mzunguko wa Uchaguzi



# SURA YA PILI

# TATHMINI YA UCHAGUZI MKUU

## 2.1. Utangulizi

Tathmini baada ya utekelezaji wa majukumu huziwezesha Taasisi kujua ni kwa jinsi gani wadau wake wa ndani na nje wanavyouona utendaji kazi wa Taasisi husika. Wadau hao hutoa maoni na mapendekezo mbalimbali ambayo huonesha maeneo ambayo taasisi imefanya vizuri na ambayo yanahitaji maboresho. Kwa kutumia matokeo ya tathmini, taasisi huweka mikakati ya kuboresha utekelezaji wa majukumu ili kufikia matarajio ya wadau wake.

Tathmini baada ya uchaguzi ni sehemu muhimu katika kukamilisha mzunguko wa uchaguzi. Baadhi ya nchi zimekuwa zikifanya tathmini baada ya kukamilisha uchaguzi mkuu kupitia Tume za Uchaguzi za nchi husika kwa lengo la kupima utendaji kazi wakati wa uchaguzi. Matokeo ya tathmini yameziwezesha Tume hizo kufanya maboresho katika utekelezaji wa programu mbalimbali za uchaguzi. Baadhi ya nchi ambazo zimefanya tathmini ni pamoja na Canada (2011), Ghana (2012), India (2019) na Kenya 2013.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mara ya kwanza ilifanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za uchaguzi katika maeneo mbalimbali nchini. Matokeo ya tathmini yalitoa picha ya jinsi ambavyo Tume iliendesha uchaguzi. Tume ilibaini maeneo ambayo yalikuwa ni muhimu kuyaboresha ili kuwa na uchaguzi bora zaidi. Baadhi ya mambo yaliyobainika na kufanyiwa kazi ni pamoja na kuongezwa kwa vituo vya kupigia kura

kutoka 65,105 vilivyokuwepo mwaka 2015 hadi 81,567 mwaka 2020, kuunganishwa kwa mifumo mbalimbali ya uchaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa kuongezewa jukumu la kutoa elimu ya uraia, kuboreshwa kwa posho za watendaji wa vituo na kuboreshwa kwa ulinzi siku ya uchaguzi.

## 2.2 Tathmini ya Uchaguzi Mkuu

Tume baada ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, imefanya tathmini ili kupata mrejesho kutoka kwa wadau kuhusu zoezi la uchaguzi mkuu lilivyoendeshwa. Tathmini hii imebainisha mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uendeshaji uchaguzi. Vilevile, kupitia zoezi la tathmini Tume imepokea maoni na mapendekezo ya wadau ya jinsi ya kuboresha utekelezaji wa majukumu yake katika chaguzi zinazofuatia.

## 2.3 Msingi wa Tathmini

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeazimia kuendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kikatiba na ya kisheria ya kusimamia na kuratibu uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani wa Tanzania Bara.

Maboresho hayo yanakusudia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika shughuli za uchaguzi ili kuleta ufanisi zaidi na kuendelea kukuza demokrasia nchini kwa kusimamia chaguzi zilizo huru, za haki na kuaminika. Hivyo, msingi mkuu wa kufanya tathmini baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulitokana na kuzingatiwa kwa mambo yafuatayo: -

### 2.3.1 Kukamilisha Mzunguko wa Uchaguzi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume huzingatia mzunguko wa uchaguzi ambao umeainisha majukumu yanayotekelezwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Tathmini ya uchaguzi ni mojawapo ya majukumu yanayotakiwa kutekelezwa baada ya uchaguzi kukamilika. Hivyo, ni muhimu kwa Tume kutekeleza jukumu hilo ili kupata mwelekeo wa maandalizi ya uchaguzi unaofuata.

### 2.3.2 Mwongozo wa Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji wa Mwaka 2014

Mwongozo wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa mwaka 2014 uliotolewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unazitaka taasisi za umma kufanya ufuatiliaji na tathmini kila baada ya kukamilisha mazoezi makubwa ya kitaifa. Hivyo, tathmini hii pamoja na mambo mengine imefanyika ili kukidhi matakwa ya mwongozo huo.

### 2.3.3 Mpango Mkakati wa Tume wa Mwaka 2016/17 - 2020/21

Tume inatekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Mpango huo umeainisha jinsi ambavyo Tume imejipanga kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tathmini imefanyika ikiwa ni utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wake.

## 2.4 Malengo ya Kufanya Tathmini

Tathmini imefanyika ili kujua hali halisi ya zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 lilivyoendeshwa. Vilevile, tathmini ililenga mambo yafuatayo: -

### 2.4.1 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilifanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa awamu mbili kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Tathmini ililenga kupata maoni kuhusu jinsi zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulivyoendeshwa na kupata mapendekezo ya kuboresha zoezi hilo kwa chaguzi zijazo.

### 2.4.2 Ushirikishwaji wa Wadau katika Mchakato wa Uchaguzi

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na sheria. Katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilishirikisha wadau mbalimbali wa uchaguzi ikiwemo Serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia, vyombo vya habari, viongozi wa dini, makundi maalum, taasisi za ulinzi na usalama na watazamaji wa uchaguzi.

Ushirikishwaji wa wadau unasaidia kuleta uwazi na kuongeza ufanisi katika shughuli za uchaguzi. Tathmini ililenga kupima ushirikishwaji wa wadau katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kubaini jinsi ushirikishwaji unavyoweza kuboreshwa katika chaguzi zijazo.

### 2.4.3 Kampeni za Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume iliratibu shughuli za kampeni za uchaguzi kwa kushirikisha vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine kwa kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi ambayo

wagombea na vyama vya siasa vilipaswa kuzingatia wakati wote wa kampeni. Vilevile, tathmini ililenga kubaini iwapo sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi vilifuatwa wakati wa uendeshaji wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 na kubaini changamoto zozote zilizojitokeza katika kipindi hicho.

### 2.4.4 Ufanisi wa Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume

Tume inasimamia na kuratibu uchaguzi kwa mujibu wa sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo mbalimbali ya Tume kwa watendaji wa uchaguzi. Sheria, kanuni na maadili ya uchaguzi yanapaswa kufuatwa na wadau wote wanaohusika kipindi chote cha mchakato wa uchaguzi. Kwa msingi huo, tathmini imefanyika ili kubaini iwapo sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume kama yalieleweka na yalisaidia katika kusimamia na kuratibu uchaguzi na iwapo yanahitaji kufanyiwa maboresho katika chaguzi zijazo.

### 2.4.5 Kupima Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura katika Mchakato wa Uchaguzi

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilitoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia njia mbalimbali kama vile vipindi vya redio, gari la matangazo la Tume, runinga, magazeti, mitandao ya kijamii, magari ya matangazo ya halmashauri na vipeperushi. Tathmini ilifanyika ili kuangalia iwapo wapiga kura walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu elimu ya mpiga kura iliyotolewa na iwapo njia zilizotumika kutoa elimu hiyo zilifikisha ujumbe uliokusudiwa.

Vile vile, tathmini ililenga kubaini iwapo muda uliotumika katika kutoa elimu ya mpiga kura ulitosha kuwaelimisha wapiga kura.

### 2.4.6 Mrejesho wa Jinsi Zoezi la Kupiga Kura Lilivyofanyika

Ufanisi wa mchakato wa kupiga kura unategemea watendaji wa vituo kufuata taratibu zilizowekwa pamoja na maelekezo ya Tume. Baadhi ya taratibu hizo ni pamoja na muda wa kufunguliwa kwa vituo vya kupigia kura, utambulisho wa mpiga kura, upangaji wa vituo vya kupigia kura na uwepo wa mawakala wa vyama vya siasa katika vituo vya kupigia kura.

Tathmini hii ililenga kubaini iwapo taratibu za kupiga kura na maelekezo ya Tume yalifuatwa ipasavyo na kubaini kama watu wenye mahitaji maalum na makundi maalum katika jamii walipewa kipaumbele. Aidha, tathmini ililenga kupata mapendekezo ya kuboresha kupiga kura kwa chaguzi zijazo.

### 2.4.7 Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo wa Wapiga Kura

Matokeo ya kura za kiti cha Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 yalibainisha kuwa kati ya wapiga kura 23,161,440 walioandikishwa, wapiga kura 15,596,110 sawa na asilimia 67.34 walijitokeza kupiga kura. Aidha, wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kati ya wapiga kura 29,754,699 walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, wapiga kura waliojitokeza kupiga kura ni 15,091,950 sawa na asilimia 50.72. Takwimu hizi zinabainisha kuwepo kwa mwitikio mdogo wa wapiga kura kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na uchaguzi uliopita wa mwaka 2015.

Tathmini ililenga kubaini sababu za baadhi ya wapiga kura walioandikishwa kupiga kura kutojitokeza siku ya uchaguzi na kupata mapendekezo ya kuboresha chaguzi zijazo. Mwitikio wa wapiga kura katika chaguzi kuu sita (6) zilizopita ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1: Mwitiko wa Wapiga Kura katika Chaguzi Mbalimbali**

| Na. | Mwaka wa Uchaguzi | Wapiga Kura walioandikishwa | Wapiga Kura Waliojitokeza kupiga Kura | | Wapiga Kura ambao hawakujitokeza kupiga Kura | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % |
| 1. | 1995 | 8,929,969 | 6,846,681 | 76.7 | 2,083,288 | 23.3 |
| 2. | 2000 | 10,088,484 | 8,517,598 | 84.43 | 1,570,886 | 15.57 |
| 3. | 2005 | 16,442,657 | 11,365,477 | 69.12 | 5,077,180 | 30.88 |
| 4. | 2010 | 20,137,303 | 8,626,303 | 42.84 | 11,511,000 | 57.16 |
| 5. | 2015 | 23,161,440 | 15,596,110 | 67.34 | 7,565,330 | 32.66 |
| 6. | 2020 | 29,754,699 | 15,091,950 | 50.72 | 14,662,749 | 49.2 |

***Chanzo:*** *Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

### 2.4.8 Uwepo wa Kura Zilizokataliwa

Uchaguzi wa kiti cha Rais wa Mwaka 2015, jumla ya kura 402,248 zilikataliwa sawa na asilimia 2.58 ya kura zote zilizopigwa, mwaka 2020 jumla ya kura 261,755 zilikataliwa sawa na asilimia 1.73 ya kura zote zilizopigwa, ikilinganishwa na asilimia 1.6 ya kiwango cha kimataifa. Pamoja na takwimu kuonesha kura zilizokataliwa zimepungua ikilingalishwa na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, bado kuna changamoto ya kuwepo kwa kura nyingi zilizokataliwa katika baadhi ya maeneo. Hivyo, tathmini ililenga kubaini sababu za kuwepo kwa kura nyingi zilizokataliwa katika baadhi ya maeneo. Jedwali Na.2 linaonesha mwenendo wa kura zilizokataliwa kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 1995 – 2020.

**Jedwali Na. 2: Kura Zilizokataliwa katika Chaguzi Mbalimbali**

| Na. | Mwaka wa Uchaguzi | Wapiga Kura walioandikishwa | Wapiga Kura Waliojitokeza kupiga Kura | | Kura Zilizoharibika/ Kataliwa | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Idadi | % | Idadi | % |
| 1. | 1995 | 8,929,969 | 6,846,681 | 76.7 | 333,936 | 4.92 |
| 2. | 2000 | 10,088,484 | 8,517,598 | 84.43 | 343,162 | 4.60 |
| 3. | 2010 | 20,137,303 | 8,626,303 | 42.84 | 227,889 | 2.65 |
| 4. | 2015 | 23,161,440 | 15,596,110 | 67.34 | 402,248 | 2.58 |
| 5. | 2020 | 29,754,699 | 15,091,950 | 50.72 | 261,755 | 1.73 |

***Chanzo:*** *Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

# SURA YA TATU

# MBINU ZILIZOTUMIKA KUFANYA TATHMINI

## 3.1 Utangulizi

Tathmini hii imefanyika kwa kutumia mbinu mbalimbali za ukusanyaji wa takwimu ambazo zimeiwezesha Tume kupata mrejesho wa jinsi Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulivyoendeshwa. Mbinu hizo ni pamoja na kuweka vigezo vya kuchagua maeneo ya tathmini, wigo na maeneo ya tathmini, njia zilizotumika kukusanya takwimu, sampuli ya waliohojiwa na uchambuzi wa takwimu.

## 3.2 Wigo na Maeneo ya Tathmini

Zoezi la tathmini lilifanyika katika mikoa 24, kati ya hiyo mikoa 22 ilikuwa ya Tanzania Bara na mikoa miwili (2) ilikuwa ya Tanzania Zanzibar. Katika mikoa hiyo yalihusika majimbo 44 ya Tanzania Bara na majimbo manne (4) ya Tanzania Zanzibar. Orodha ya mikoa na halmashauri zilizofanyiwa tathmini ni kama inavyooneshwa kwenye kiambatisho Na.1.

Tathmini hii ilifanyika kuanzia Novemba hadi Disemba, 2020 na iliangazia mchakato wa uchaguzi kuanzia hatua ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, uteuzi wa wagombea, kupiga kura hadi kujumlisha na kutangaza matokeo.

Katika zoezi hili Tume ilifanya mikutano na watendaji wa uchaguzi ambao ni waratibu wa uchaguzi mikoa, wasimamizi wa uchaguzi, maafisa uchaguzi na maafisa ugavi. Vilevile, kulikuwa na mahojiano ya ana kwa ana na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata,

wasimamizi wa vituo vya kupigia kura, viongozi wa vyama vya siasa na wapiga kura. Pia, kulikuwa na majadiliano na makundi maalum katika jamii ikiwemo wazee, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Aidha, tathmini ilipitia taarifa zilizowasilishwa na taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura pamoja na taarifa za watazamaji wa uchaguzi wa ndani na wa kimataifa.

### 3.3 Vigezo Vilivyotumika Kuchagua Maeneo ya Tathmini

Kabla ya kuanza kwa zoezi la Tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliweka vigezo vya kuchagua maeneo ya kufanyia tathmini. Vigezo vilivyowekwa vilizingatia mambo yafuatayo: -

(i) mwitikio wa wapiga kura (mwitikio mdogo, wa wastani na mkubwa);

(ii)idadi ya kura zilizokataliwa; na

(iii) uwakilishi wa kanda zote za uchaguzi.

Vigezo hivyo vimeinishwa katika Mpango Mkakati wa Tume (*NEC Strategic Plan*) wa kipindi cha 2016/17 – 2020/21, kwamba katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, mwitikio wa wapiga kura ufikie angalau asilimia 71 na kura zilizokataliwa zisizidi asilimia 1.6.

Katika zoezi hili la tathmini, mwitikio wa wapiga kura umeangaliwa kupitia kura za kiti cha Rais. Kwa madhumuini ya tathmini hii, mgawanyo wa mwitikio wa wapiga kura ulipendekezwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Mgawanyo wa Mwitikio wa Wapiga Kura**

| Na. | Aina ya Mwitikio | Asilimia |
|---|---|---|
| 1. | Mdogo | 0 - 50 |
| 2. | Wastani | 51 - 70 |
| 3. | Mkubwa | 71 - 100 |

### 3.3.1 Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo

Maeneo yaliyokuwa na mwitikio mdogo wa wapiga kura ni maeneo yaliyokuwa na asilimia 0 hadi 50 ya wapiga kura waliojitokeza ikilinganishwa na idadi ya wapiga kura waliojiandikisha kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa kuzingatia kigezo hiki majimbo 13 katika mikoa 12 yalichaguliwa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.4.

**Jedwali Na. 4: Maeneo Yenye Mwitikio Mdogo**

| Mkoa | Na. | Jimbo | Wapiga Kura Waliondikishwa | Wapiga Kura Waliopiga Kura | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| TABORA | 1. | Tabora Mjini | 181,757 | 54,964 | 30.24 |
| | 2. | Nzega Mjini | 63,691 | 19,571 | 30.73 |
| MWANZA | 3. | Nyamagana | 348,891 | 122,990 | 35.25 |
| PWANI | 4. | Kibaha Vijijini | 71,236 | 25,199 | 35.37 |
| ARUSHA | 5. | Arusha Mjini | 374,281 | 133,307 | 35.62 |
| TANGA | 6. | Korogwe Vijijini | 141,207 | 67,333 | 47.68 |
| RUVUMA | 7. | Songea Mjini | 151,394 | 61,448 | 43.23 |
| NJOMBE | 8. | Makambako | 71,372 | 30,987 | 43.42 |
| MBEYA | 9. | Mbeya Vijijini | 184,495 | 81,992 | 44.28 |
| SONGWE | 10. | Vwawa | 124,554 | 56,250 | 45.27 |
| IRINGA | 11. | Iringa Mjini | 126,099 | 56,449 | 45.16 |
| KIGOMA | 12. | Kigoma Kaskazini | 119,418 | 55,692 | 46.64 |
| RUKWA | 13. | Kalambo | 128,498 | 59,972 | 46.67 |

***Chanzo:*** *Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2020*

### 3.3.2 Maeneo Yenye Mwitikio wa Wastani

Maeneo yaliyokuwa na mwitikio wa wastani wa wapiga kura ni maeneo yaliyokuwa na mwitikio wa wapiga kura kati ya asilimia 51 hadi 70 ikilinganishwa na idadi ya wapiga kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Majimbo 7 yaliyopo katika mikoa 5 yalichaguliwa kwa kuzingatia kigezo hiki kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.5.

**Jedwali Na. 5: Maeneo Yenye Mwitikio wa Wastani**

| Mkoa | Na. | Jimbo | Wapiga Kura Walioandikishwa | Wapiga Kura Waliopiga Kura | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| SIMIYU | 1. | Itilima | 168,285 | 86,748 | 51.55 |
| | 2. | Bariadi | 59,121 | 30,863 | 52.20 |
| LINDI | 3. | Lindi Mjini | 251,274 | 132,649 | 52.79 |
| | 4. | Mtama | 91,844 | 50,188 | 54.64 |
| IRINGA | 5. | Kilolo | 132,339 | 75,575 | 57.11 |
| SONGWE | 6. | Tunduma | 97,856 | 57,383 | 58.64 |
| MWANZA | 7. | Ilemela | 302,552 | 178,333 | 58.94 |

***Chanzo:*** *Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2020*

### 3.3.3 Maeneo Yenye Mwitikio Mkubwa

Maeneo yaliyokuwa na mwitikio mkubwa wa wapiga kura ni maeneo yaliyokuwa na mwitikio wa wapiga kura kati ya asilimia 71 hadi 100 ikilinganishwa na idadi ya wapiga kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Majimbo 7 katika mikoa 6 yalichaguliwa kutokana na kigezo hiki kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.6.

**Jedwali Na. 6: Maeneo Yenye Mwitikio Mkubwa**

| Mkoa | Na. | Jimbo | Wapiga Kura Walioandikishwa | Wapiga Kura Waliopiga Kura | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| MJINI MAGHARIBI | 1. | Amani | 12,048 | 8,499 | 70.54 |
| DAR ES SALAAM | 2. | Temeke | 478,630 | 350,431 | 73.22 |
| MOROGORO | 3. | Morogoro Mjini | 286,840 | 233,173 | 81.29 |
| | 4. | Mvomero | 206,590 | 181,269 | 87.74 |
| MJINI MAGHARIBI | 5. | Bububu | 14,722 | 11,587 | 78.71 |
| SHINYANGA | 6. | Kahama Mjini | 216,579 | 211,588 | 97.70 |
| KILIMANJARO | 7. | Hai | 133,897 | 117,829 | 88.00 |

***Chanzo:** Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

### 3.3.4 Maeneo Yenye Kura nyingi Zilizokataliwa


Maeneo yaliyokuwa na kura nyingi zilizokataliwa ni maeneo ambayo yalikuwa na zaidi ya asilimia 1.6 ya kura zilizokataliwa ikilinganishwa na kura zote zilizopigwa katika jimbo husika. Kwa kutumia kigezo hiki majimbo 8 katika mikoa 7 yalichaguliwa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 7.

**Jedwali Na. 7: Maeneo Yenye Kura nyingi Zilizokataliwa**

| Mkoa | Na. | Jimbo | Asilimia ya Kura zilizokataliwa |
|---|---|---|---|
| Geita | 1. | Geita Mjini | 2.74 |
| | 2. | Geita Vijijini | 2.83 |
| Kusini Pemba | 3. | Chakechake | 2.87 |
| Singida | 4. | Singida Mashariki | 3.04 |
| Mtwara | 5. | Mtwara Vijijini | 3.43 |
| Lindi | 6. | Mtama | 3.45 |
| Dodoma | 7. | Bahi | 3.77 |
| Kusini Pemba | 8. | Chonga | 5.70 |

***Chanzo:** Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2020*

**Mchoro Na. 2: Majimbo Yaliyofanyiwa Tathmini**




### 3.4 Njia Zilizotumika Kukusanya Takwimu

Tume ilitumia njia mbalimbali katika kukusanya takwimu ambazo zilizotumika kutoa matokeo ya tathmini. Njia hizo ni pamoja na mahojiano ya ana kwa ana, ujazaji wa madodoso na majadiliano na makundi maalum katika jamii. Njia nyingine zilikuwa ni kufanya mapitio ya nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na taarifa za watazamaji wa uchaguzi, taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura na mikutano iliyowahusisha watendaji wa uchaguzi.

#### 3.4.1 Mahojiano ya Ana kwa Ana

Mahojiano ya ana kwa ana yalifanyika kwa kutumia madodoso ya aina tatu ambayo yalikuwa yameandaliwa kwa ajili ya watendaji wa uchaguzi, viongozi wa vyama vya siasa na wapiga kura. Kila dodoso lilikuwa na maswali yaliyoandaliwa ili kupata taarifa zilizokusudiwa. Maswali hayo yalilenga kubaini iwapo:-

(i) sheria za uchaguzi, kanuni, maadili ya uchaguzi pamoja na miongozo na maelekezo mbalimbali ya Tume yalisaidia katika kuendesha uchaguzi;

(ii) upatikanaji wa taarifa za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulivyokuwa;

(iii) elimu ya mpiga kura ilitolewa ipasavyo kipindi cha uchaguzi mkuu na ilieleweka kwa wadau;

(iv) siku ya kupiga kura, watu wenye mahitaji maalum na makundi mbalimbali katika jamii walipewa vipaumbele;

(v) wadau walishirikishwa katika mchakato wa uchaguzi kwa jinsi inayofaa;

(vi) taratibu za uchaguzi zilifuatwa na watendaji wa uchaguzi;

(vii) namna kampeni za uchaguzi zilivyoendeshwa;

(viii) iwapo vifaa vya uchaguzi vilikidhi mahitaji na vilikuwa na ubora unaotakiwa;

(ix) kama mawakala wa vyama vya siasa waliapishwa, changamoto za uapishaji na iwapo walitekeleza majukumu yao;

(x) mazingira yaliyozunguka vituo vya kupigia kura yalikuwa rafiki na salama na wapiga kura walifika vituoni kwa urahisi;

(xi) kufunguliwa na kufungwa kwa vituo vya kupigia kura na changamoto zilizojitokeza;

(xii) kuhesabu kura na kutangaza matokea na changamoto zilizojitokeza

(xiii) kuna sababu za kupungua kwa mwitikio wa wapiga kura kutoka 67.34 asilimia mwaka 2015 hadi 50.72 asilimia mwaka 2020;

(xiv) wadau wa uchaguzi waliridhika na utendaji wa watendaji wa uchaguzi katika kushughulikia uteuzi wa wagombea; na

(xv) kupata maoni ya wadau juu mchakato wa uchaguzi ulivyoendeshwa.

Zifuatazo ni baadhi ya picha za mahojiano ya ana kwa ana yaliyofanyika kwenye baadhi ya mikoa.



*Afisa wa Tume Bi. Rose Msaki (aliyesimama) akiwaongoza viongozi wa vyama vya siasa kujaza madodoso – Mkoani Arusha*



*Afisa wa Tume Ndugu Richard Lugomela (wa kwanza kulia) akifanya mahojiano ya ana kwa ana na wapiga kura Mkoani Tabora*

### 3.4.2 Majadiliano na Makundi Maalum

Majadiliano na makundi maalum yalijumuisha makundi ya wazee, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Majadiliano yalifanyika kwenye makundi hayo manne (4) kwa idadi tofauti kwa kuzingatia maeneo yaliyofanyiwa tathmini. Katika majadiliano hayo, jumla ya mikoa 24 ilichaguliwa ambapo mikoa sita (6) ilihusishwa katika kujadiliana na makundi ya wazee, mikoa saba (7) vijana, mikoa sita (6) wanawake na mikoa mitano (5) watu wenye ulemavu. Njia ya sampuli nasibu (*random sampling method*) ilitumika kuchagua mikoa kwa ajili ya kufanya majadiliano na mojawapo ya kundi maalum. Mikoa na makundi yaliyofanya majadiliano yanaonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Aina ya Makundi Maalum Yaliyofanya Majadiliano**

| Na. | Mikoa | Kundi |
|---|---|---|
| 1. | Arusha | Wazee |
| 2. | Kilimanjaro | |
| 3. | Singida | |
| 4. | Dodoma | |
| 5. | Tabora | |
| 6. | Kigoma | |
| 7. | Rukwa | Wanawake |
| 8. | Iringa | |
| 9. | Njombe | |
| 10. | Mbeya | |
| 11. | Ruvuma | |
| 12. | Mwanza | |
| 13. | Lindi | Vijana |
| 14. | Mtwara | |
| 15. | Morogoro | |
| 16. | Pwani | |
| 17. | Dar es Salaam | |
| 18. | Tanga | |
| 19. | Simiyu | |
| 20. | Shinyanga | Watu wenye ulemavu |
| 21. | Geita | |
| 22. | Songwe | |
| 23. | Mjini Magharibi | |
| 24. | Kusini Pemba | |

Aidha, kila kundi lilijumuisha watu saba (7) kwa mchanganyiko wa wanaume na wanawake. Majadiliano hayo yalilenga mambo yafuatayo: -

(i) maoni kuhusu mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika vipengele vya uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, utambulisho wa mawakala wa vyama vya siasa katika vituo vya kupigia kura, kupiga kura na kutangaza matokeo;

(ii) sababu za kupungua kwa mwitikio wa wapiga kura kutoka asilimia 67.34 kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 hadi asilimia 50.72 kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020;

(iii) ushauri wa wadau wa uchaguzi kwa Tume katika kuboresha chaguzi nyingine zinazofuata ili mwitikio wa wapiga kura uwe mkubwa;

(iv) kubaini mambo yanayoweza kufanywa na Tume ili kuwezesha umma kuwa na uelewa wa Tume inavyofanya kazi;

(v) masuala gani yalifanyika sawa na ambayo hayakufanyika sawa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020;

(vi) masuala yanayotakiwa kuboreshwa katika mchakato mzima wa uchaguzi unaoendeshwa na Tume; na

(vii) masuala mengine muhimu ambayo wadau wa uchaguzi wanapendekeza ili Tume iyatilie mkazo katika kuyatatua.



*Afisa wa Tume Bi. Josephine Mchalange (wa kwanza kushoto) akifanya mahojiano na kundi la Wanawake wakati wa Tathnimi ya Uchaguzi Mkuu, 2020 mkoani Mwanza*

### 3.4.3 Mikutano na Watendaji wa Uchaguzi

Tume ilifanya mikutano na waratibu wa uchaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi, maafisa uchaguzi na maafisa ugavi kutoka katika halmashauri na wilaya zote nchini kwa lengo la kupata mrejesho wa jinsi uchaguzi ulivyoendeshwa katika maeneo yao. Katika mikutano hiyo, watendaji walipata fursa ya kujadili katika

makundi na kubaini changamoto walizokutana nazo na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha chaguzi zijazo. Kupitia mikutano hiyo, wahusika walijaza bango kitita lililowaongoza kutoa maoni na mapendekezo yao katika kila hatua ya mchakato wa uchaguzi.




*Watendaji wa uchaguzi wakiwa katika mkutano wa pamoja na viongozi wa Tume (hawapo katika picha) wakati wa Tathmini ya Uchaguzi Mkuu, 2020 katika ukumbi wa Morena Hotel - Dodoma mnamo tarehe 20 Novemba, 2020*



*Wajumbe na Katibu wa Tume (wa pili kutoka kushoto) wakiongoza mkutano kati yao na watendaji wa Uchaguzi Mkuu, 2020 (hawapo katika picha) kuhusu Tathmini Mkutano ulifanyika Morena Hotel - Dodoma, Tarehe 20 Novemba, 2020*

### 3.4.4 Mapitio ya Nyaraka

Katika kukusanya taarifa, Tume ilifanya mapitio ya taarifa za chaguzi mbalimbali. Taarifa hizo ni pamoja na taarifa za watazamaji wa uchaguzi, taarifa za taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura, taarifa ya utekelezaji wa shughuli za uchaguzi kutoka katika mikoa na halmashauri mbalimbali na taarifa za chaguzi kuu zilizopita.

## 3.5 Sampuli ya Waliohojiwa

Katika tathmini hii, sampuli ya watu waliohojiwa ilikuwa 1,874 ambapo 1,706 walijaza madodoso na 168 walishiriki majadiliano ya makundi maalum. Kati watu 1,706 walihojiwa kwa kutumia madodoso, 954 walikuwa watendaji wa uchaguzi, 445 wapiga kura na 307 walikuwa viongozi wa vyama vya siasa.

Aidha, kati ya watu waliohojiwa wanaume walikuwa 1,176 sawa na asilimia 62.8 na wanawake walikuwa 698 sawa na asilimia 37.2 ya watu wote waliohojiwa. Mchanganuo wa waliohojiwa ni kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9: Sampuli ya Waliohojiwa kwa Jinsi**

| Na. | Waliohojiwa | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Wanaume | Wanawake | |
| 1. | Watendaji wa Uchaguzi | 637 | 317 | 954 |
| 2. | Wapiga kura | 244 | 201 | 445 |
| 3. | Viongozi wa Vyama vya Siasa | 238 | 69 | 307 |
| 4. | Makundi Maalum | 57 | 111 | 168 |
| **Jumla** | | **1,176** | **698** | **1,874** |

Aidha, kwa kutumia mahojiano kwa njia ya dodoso, mchanganuo wa waliohojiwa kwa kuzingatia umri unaonesha kuwa vijana (miaka 18 – 35) walikuwa 596 sawa na asilimia 34.9, wenye umri kati ya miaka 36 – 60 walikuwa 1,000 sawa na asilimia 58.6 na umri zaidi ya miaka 60 walikuwa 110 sawa na asilimia 6.5. Mchanganuo huo umeoneshwa katika Jedwali Na.10.

**Jedwali Na. 10: Mgawanyo wa Waliohojiwa kwa Umri**

| Na. | Waliohojiwa | Umri | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 18-35 | 36-60 | Zaidi 60 | |
| 1. | Watendaji wa Uchaguzi | 338 | 579 | 37 | **954** |
| 2. | Wapiga kura | 187 | 208 | 50 | **445** |
| 3. | Viongozi wa Vyama vya Siasa | 71 | 213 | 23 | **307** |
| **Jumla** | | **596** | **1000** | **110** | **1,706** |

## 3.6 Uchambuzi wa Takwimu

Uchambuzi wa takwimu ulifanyika kwa kuandaa *template* za dodoso zote tatu kwenye mfumo wa takwimu wa *Statistical Package for the Social Sciences* (SPSS), kukagua madodoso ili kuangalia ujazaji, kuyapa mageresho majibu ya maswali yaliyohitaji ufafanuzi au yenye majibu ya kujieleza, kuingiza takwimu kwenye mfumo huo na kufanya marekebisho yaliyotokana na makosa ya kimfumo.

# SURA YA NNE

# MATOKEO YA TATHMINI

## 4.1 Utangulizi

Matokeo ya tathmini iliyofanyika baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, yametokana na takwimu zilizokusanywa kutoka makundi mbalimbali yaliyofikiwa. Makundi hayo yanajumuisha vyama vya siasa, wapiga kura, makundi maalum katika jamii na watendaji wa uchaguzi. Watendaji hao ni pamoja na waratibu wa uchaguzi wa mikoa, wasimamizi wa uchaguzi, wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata, maafisa uchaguzi na watendaji wa vituo. Maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yalifanyiwa tathmini ili kupata mrejesho wa jinsi Tume ilivyoendesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Maeneo hayo ni pamoja na ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi, kuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, kupiga kura, mwitikio wa wapiga kura, kuhesabu kura pamoja na kujumlisha na kutangaza matokeo. Matokeo ya tathmini katika maeneo hayo ni yafuatayo:-

## 4.2 Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume

Tume katika kusimamia na kuratibu uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, iliongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa


(Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2020 na maelekezo mbalimbali ya Tume. Maelekezo hayo yalitolewa kwa vyama vya siasa na wagombea, mawakala wa vyama vya siasa, wasimamizi wa uchaguzi, makarani waongozaji na wasimamizi wa vituo vya kupigia kura.

Tathmini ililenga kubaini endapo sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo kwa wadau na watendaji wa uchaguzi yaliyotolewa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 yalisaidia katika kuendesha uchaguzi na kama yalieleweka kwa wadau.

Kati ya viongozi wa vyama vya siasa na watendaji wa uchaguzi 1,261 waliohojiwa, 1,241 sawa na asilimia 98.4 walisema kuwa sheria, kanuni, maadili na vitabu vya maelekezo kwa wadau wa uchaguzi vilisaidia katika kuendesha uchaguzi. Aidha, waliohojiwa 20 sawa na asilimia 1.6 walisema kuwa sheria, kanuni, maadili na vitabu vya maelekezo havikusaidia katika kuendesha uchaguzi. Matokeo haya yanaonesha kuwa sheria, kanuni na maelekezo kwa wadau wa uchaguzi yalisaidia katika kuendesha uchaguzi.

Aidha, kuhusu kueleweka kwa sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume, viongozi wa vyama vya siasa na watendaji 1,063 waliohojiwa, sawa na asilimia 84.3 walisema sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa na Tume yalieleweka vizuri, wakati waliohojiwa 198 sawa na asilimia 15.7 walieleza kuwa sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa na Tume hayakueleweka kwa wadau. Chati Na. 1 inaonesha matokeo ya tathmini kuhusu kueleweka kwa sheria, kanuni maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume.

**Chati Na. 1: Kueleweka kwa Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume**




Matokeo haya yanaonesha kuwa sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya uchaguzi yaliyotumika katika kuratibu na kusimamia uendeshaji wa uchaguzi yalieleweka kwa wadau wengi wa uchaguzi na yalisaidia katika kuendesha Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Waliohojiwa walipendekeza sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo mbalimbali ya Tume yafanyiwe maboresho kama ifuatavyo: -

(i) sheria na kanuni za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili zieleweke kwa urahisi kwa wadau;

(ii) kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kuwa na sheria moja ya kusimamia na kuratibu uchaguzi;

(iii) kuangalia upya sifa za wagombea Ubunge na Udiwani hususan kipengele cha elimu ili kukiboresha;

(iv) sheria ya uchaguzi ya serikali za mitaa ifafanue zaidi kuhusiana na mkazi wa kawaida katika eneo la sifa za wagombea Udiwani, ikiwezekana mgombea huyo awe mkazi wa kata anayogombea;

(v) viwango vya adhabu kwa watendaji wa uchaguzi na vyama vya siasa vinavyokiuka sheria viongezwe;

(vi) afisa uchaguzi atambuliwe na sheria za uchaguzi kama mtendaji wa uchaguzi kama ilivyo kwa watendaji wengine wa uchaguzi;

(vii) wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na kata waruhusiwe kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa;

(viii) wapiga kura waruhusiwe kupiga kura ya Rais katika kituo chochote tofauti na ilivyo sasa ambapo mpiga kura anaruhusiwa kupiga kura katika kituo alichojiandikisha tu;

(ix) kampeni za nyumba kwa nyumba ziwekewe utaratibu ili zisiwe chanzo cha vurugu;

(x) muda wa kufungua na kufunga vituo vya kupigia kura ubadilishwe, zoezi la kupiga kura lianze saa 12 asubuhi badala ya saa moja asubuhi; na

(xi) Tume iwe na watendaji wake hadi ngazi za halmashauri.

### 4.3 Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

Wakati wa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilifanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa awamu mbili kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Taifa

ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 21(5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Tathmini ililenga kupata maoni kuhusu upatikanaji wa taarifa za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ulivyokuwa. Maoni hayo yalijikita katika maeneo yafuatayo: -

(i) ufanisi wa mashine za kuandikishia wapiga kura (BVR);

(ii) upatikanaji wa kadi za mpiga kura;

(iii) kupata taarifa kuhusu utoshelevu wa muda wa kujiandikisha;

(iv) uhakiki wa taarifa wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura;

(v) njia zilizotumika kuhakiki taarifa za mpiga kura wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura;

(vi) changamoto zilizojitokeza wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na

(vii) mchakato wa uandikishaji katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

### 4.3.1 Ufanisi wa Mashine za Kuandikishia Wapiga Kura kwa Kutumia Alama za Kibaiolojia - BVR

Waliohojiwa 1,706 walitoa maoni kuhusu ufanisi wa mashine za BVR katika kuandikisha wapiga kura. Kati ya hao, 954 walikuwa watendaji wa uboreshaji na 752 walikuwa wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa. Watendaji 942 kati ya 954 ya waliohojiwa ikiwa ni sawa na asilimia 98.7 walieleza kuwa mashine hizo zilifanya kazi ipasavyo na

watendaji 12 sawa na asilimia 1.3 walisema kuna wakati mashine za BVR zilishindwa kufanya kazi ipasavyo.

Waliohojiwa 467 kati ya 752 ambao ni wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa sawa na asilimia 62.1 walieleza kuwa mashine hizo zilifanya kazi ipasavyo na waliohojiwa 285 sawa na asilimia 37.9 walisema kuna wakati mashine za BVR zilishindwa kufanya kazi ipasavyo. Matokeo haya yanaonesha kuwa mashine za BVR kwa kiwango kikubwa zilifanya kazi kwa ufanisi wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

### 4.3.2 Upatikanaji wa Kadi ya Mpiga Kura


Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 752 walihojiwa kuhusu upatikanaji wa kadi ya mpiga kura. Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 640 kati ya 752 ya waliohojiwa sawa na asilimia 85.1 walisema upatikanaji wa kadi ya mpiga kura ulikuwa rahisi na 112 sawa na asilimia 14.9 walisema upatikanaji wa kadi ya mpiga kura haukuwa rahisi.

### 4.3.3 Muda wa Kujiandikisha

Viongozi wa vyama vya siasa, wapiga kura na watendaji wa uboreshaji 1,706 waliulizwa kuhusu muda wa kujiandikisha au kuboresha taarifa za wapiga kura kituoni. Matokeo yanaonesha kuwa, waliohojiwa 1,104, kati ya 1,706 sawa na asilimia 64.7 walibainisha kuwa, muda wa uandikishaji uliowekwa na Tume ulitosha, waliohojiwa 561 sawa na asilimia 32.9 walisema kuwa muda wa uandikishaji haukutosha na waliohojiwa ambao ni 41 sawa na asilimia

2.4 walieleza kuwa, hawafahamu kama muda huo haukutosha au hautoshi. Ufafanuzi umetolewa katika Chati Na. 2.

**Chati Na. 2: Muda wa Kujiandikisha**




Matokeo haya yanaonesha kuwa, muda uliowekwa na Tume kwa ajili ya zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unahitaji kuongezwa ili kutoa fursa kwa wapiga kura wengi zaidi kujiandikisha au kuboresha taarifa zao.

### 4.3.4 Uhakiki wa Taarifa wakati wa Uwekaji wazi wa Daftari la Awali

Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 752 waliulizwa endapo walihakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura. Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 601 kati ya 752 waliohojiwa sawa na asilimia 79.9 walisema walihakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura na 151 sawa na asilimia 20.1 walisema hawakuhakiki taarifa zao.

Matokeo haya yanaonesha kuwa, idadi kubwa ya wapiga kura walihakiki taarifa zao.

Vilevile, kwa wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliohojiwa na kutoa maoni yao kuhusu kutohakiki taarifa zao wakati wa uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura, walitoa sababu mbalimbali za kutohakiki taarifa zao. Baadhi ya sababu walizotoa ni pamoja na: -

(i) kuwa na majukumu mengi hivyo kukosa muda wa kuhakiki;

(ii) kutokupata taarifa kuhusiana na zoezi la kuhakiki taarifa za mpiga kura;

(iii) kutojua sehemu ambapo Daftari la Awali la Wapiga Kura lilibandikwa;

(iv) umbali kati ya kituo cha kujiandikishia na makazi ya wapiga kura; na

(v) siku chache zilizotengwa kwa ajili ya zoezi la uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura.

### 4.3.5 Njia Zilizotumika Kuhakiki Taarifa za Mpiga Kura

Watu waliohojiwa ambao walihakiki taarifa zao, waliulizwa pia njia ambazo walitumia kuhakiki taarifa zao. Viongozi wa vyama vya siasa na wapiga kura 548 kati ya 601 ya waliohakiki taarifa zao sawa na asilimia 91.2 walisema walitumia njia ya kwenda vituoni, ambapo watu 31 waliohojiwa sawa na asilimia 5.1 walitumia njia ya simu za mkononi na watu 22 waliohojiwa sawa na asilimia 3.7 walitumia tovuti ya Tume kuhakiki taarifa zao. Matokeo haya yanaonesha kuwa,

wapiga kura wengi walikwenda kituoni moja kwa moja kuhakiki taarifa zao. Aidha, matokeo haya pia, yanaonesha kuwepo kwa njia za kielektroniki kulitoa njia mbadala kwa wapiga kura kuhakiki taarifa zao.

### 4.3.6 Changamoto Wakati wa Uboreshaji

Waliohojiwa walitakiwa kuainisha changamoto walizokutana nazo katika zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Changamoto walizoainisha katika maeneo yao ni pamoja na:-

(i) baadhi ya mashine za kuandikisha (BVR-Kits) zilikuwa na changamoto ya kutofanya kazi na nyingine ziliharibika;

(ii) baadhi ya wananchi walilalamikia suala la vituo vya kuboresha taarifa za wapiga kura kuwa mbali na makazi ya wananchi hasa wakati wa uboreshaji wa Daftari Awamu ya Pili;

(iii) baadhi ya vituo vya kuboreshea taarifa za wapiga kura kuwa na watu wengi zaidi siku za mwisho;

(iv) baadhi ya wananchi hawakuona taarifa zao kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura;

(v) baadhi ya orodha ya watu waliojiandikisha zaidi ya mara moja haikupelekwa kwa wakati kwa baadhi ya vituo;

(vi) baadhi ya wapiga kura walikuwa na kadi lakini majina yao hayakuwepo kwenye orodha ya wapiga kura;

(vii) baadhi ya wananchi waliohama na kuboresha taarifa zao kuendelea kuonekana katika vituo vyao vya awali;

(viii) baadhi ya vituo vya kuandikishia wapiga kura karatasi zilizobandikwa kwa ajili ya uhakiki zilichanwa;

(ix) baadhi ya wananchi kuonekana kukosa vigezo vya kujiandikisha na wengine kujiandikisha mara mbili; na

(x) baadhi ya wananchi walishindwa kujiandikisha kutokana na muda kuwa mchache na foleni ndefu.

### 4.3.7 Maoni Kuhusu Mchakato wa Uboreshaji

Wakati wa mahojiano, maoni mbalimbali yalitolewa kuhusu mwenendo wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika awamu zote mbili kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.

Vilevile, waliohojiwa walitoa mapendekezo mbalimbali ambayo yatasaidia kuboresha mazoezi mengine yajayo ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Baadhi ya maoni ambayo yalitolewa na wadau hao ni haya yafuatayo:-

(i) Tume iweke mfumo ili wananchi waweze kujiandikisha kwa njia ya mtandao (*Online Registration*);

(ii) elimu ya mpiga kura na uhamasishaji ifanyike ipasavyo kabla na wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na

(iii) mashine za kuandikisha wapiga kura (BVR) ziongezwe kwenye vituo ili kupunguza foleni.

## 4.4 Elimu ya Mpiga Kura

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 imepewa mamlaka ya kutoa elimu ya mpiga kura na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu hiyo. Wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume ilitumia njia mbalimbali kutoa elimu ya mpiga kura zikiwemo vyombo vya habari, mikutano na wadau, mikutano ya hadhara, gari la elimu ya mpiga kura la Tume, magari ya matangazo ya halmashauri, maonesho mbalimbali ya kitaifa, uchaguzi wa mfano (*Mock Election*) na machapisho mbalimbali.

Vilevile, Tume ilitoa vibali kwa taasisi na asasi za kiraia 252 kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo mbalimbali nchini. Tathmini ililenga kubaini endapo:-

(i) muda wa kutoa elimu ya mpiga kura ulitosha;

(ii) vifaa vya elimu ya mpiga kura vilikuwepo katika maeneo ya uchaguzi na kama ujumbe uliotolewa ulikidhi mahitaji;

(iii) njia zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura kwa jamii zilifaa;

(iv) wapiga kura walikuwa na uelewa wa haki ya kupiga kura na kubaini njia ambazo Tume inaweza kuzitumia katika chaguzi zijazo wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

(v) kuna mapendekezo ya kuboresha utoaji wa elimu ya mpiga kura.

### 4.4.1 Muda wa Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Wapiga kura 445 walihojiwa kuhusu muda unaotumika kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu. Watu 357 waliohojiwa kati ya 445 ambao ni sawa na asilimia 80.2 walieleza kuwa, muda wa kutoa elimu ya mpiga kura ulitosheleza na wapiga kura 88 ambao ni sawa na asalimia 19.8 walieleza kuwa muda wa kutoa elimu ya mpiga kura haukutosha kumuelimisha mpiga kura.

Matokeo haya yanaonesha kuwa muda uliotumika kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulitosheleza mahitaji ya wapiga kura. Hata hivyo, waliohojiwa walipendekeza Tume ifanye suala la utoaji wa elimu ya mpiga kura kuwa endelevu na elimu isitolewe wakati wa uchaguzi pekee.

### 4.4.2 Vifaa vya Elimu ya Mpiga Kura

Wapiga kura 445 walihojiwa iwapo waliwahi kuona vifaa vilivyotumika kutoa elimu ya mpiga kura vikiwemo mabango, vipeperushi na magari ya matangazo. Wapiga kura 394 kati ya 445 waliohojiwa sawa na asilimia 88.5 walieleza kuwa waliona vifaa vilivyotumika katika kutoa elimu ya mpiga kura na wapiga kura 51 ambao ni sawa na asilimia 11.5 walieleza kuwa hawakuona vifaa vya elimu ya mpiga kura.

### 4.4.3 Njia Zilizotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Wapiga kura 445 walihojiwa kuhusu kufaa au kutokufaa kwa njia zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu. Wapiga kura 403 kati ya 445 waliohojiwa sawa na asilimia 90.6 walieleza kuwa njia zilizotumika kutoa elimu ya mpiga

kura zilikuwa zinafaa, wakati wapiga kura 42 ambao ni sawa na asilimia 9.4 walieleza kuwa njia zilizotumika zilikuwa hazifai. Matokeo haya yanaonesha kuwa njia zilizotumika katika kutoa elimu ya mpiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 zilikuwa zinafaa katika maeneo mengi.

Aidha, Wapiga kura 445 walihojiwa pia kuhusu ufanisi wa njia mbalimbali zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu. Wapiga kura 102 kati ya 445 waliohojiwa sawa na asilimia 22.8 walionesha kuwa njia ya redio ni njia yenye ufanisi mkubwa na wapiga kura 80 sawa na asilimia 18.2 walisema njia ya runinga ina ufanisi mkubwa katika kutoa elimu ya mpiga kura. Ufanisi wa njia nyingine zilizotumika kutoa elimu ya mpiga kura ni kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11: Ufanisi wa Njia Zilizotumika Kutoa Elimu ya Mpiga Kura**


| Njia za Utoaji Ujumbe | Waliohojiwa | Asilimia |
|---|---|---|
| Redio | 102 | 22.8 |
| Runinga | 80 | 18.2 |
| Machapisho mbalimbali | 71 | 16.0 |
| Mitandao ya kijamii | 53 | 12.0 |
| Ujumbe mfupi wa maandishi (sms) | 52 | 11.6 |
| Magazeti | 46 | 10.4 |
| Tovuti ya tume | 40 | 9.0 |
| **Jumla** | **445** | **100** |

Matokeo yanaonesha kuwa, njia za redio, runinga, machapisho mbalimbali ziliwafikia watu wengi.

#### 4.4.4 Uelewa wa Haki ya Kupiga Kura

Wapiga kura 445 walihojiwa iwapo walikuwa na uelewa wa haki ya kupiga kura ili kuchagua kiongozi wanayemtaka. Wapiga kura 385 kati ya 445 waliohojiwa ambao ni sawa na asilimia 86.5 walieleza kuwa, walikuwa na uelewa wa haki ya kupiga kura na wapiga kura 60 sawa na asilimia 13.5 walieleza kuwa hawana uelewa wa haki ya kupiga kura kama inavyooneshwa katika Chati Na.3.

**Chati Na. 3: Uelewa wa Haki ya Kupiga Kura**




Matokeo haya yanaonesha kuwa wapiga kura katika maeneo mengi wana uelewa wa haki ya kupiga kura. Hata hivyo, elimu zaidi inahitajika ili kuwafanya wapiga kura wachache ambao hawana uelewa wapate uelewa huo.

### 4.4.5 Mapendekezo ya Kuboresha Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura

Wakati wa mahojiano ya ana kwa ana na majadiliano ya makundi maalum ya wazee, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu waliohojiwa walipendekeza Tume ifanye yafuatayo:-

(i) iandae semina na warsha mbalimbali kuhusiana na masuala ya uchaguzi;

(ii) Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha kifedha asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi;

(iii) itoe vibali kwa taasisi na asasi zenye vigezo vya kutoa elimu ya mpiga kura;

(iv) iendelee kutoa elimu ya mpiga kura katika taasisi za elimu;

(v) kwa kushirikiana na Serikali iandae mtaala wa utoaji wa elimu ya mpiga kura;

(vi) iwatumie wakalimani wa lugha za alama katika kutoa elimu ya mpiga kura;

(vii) iandae na kuongeza vifaa vya elimu ya mpiga kura kama vile machapisho mbalimbali;

(viii) elimu ya mpiga kura iwe endelevu;

(ix) itoe elimu ya mpiga kura katika maeneo yote hadi vijijini;

(x) itenge fedha kwa ajili ya halmashauri kutoa elimu ya mpiga kura kila mwaka;

(xi) iwashirikishe wadau wote muhimu katika hatua zote za uchaguzi;

(xii) ijitangaze kwa umma muda wote na sio kipindi cha uchaguzi pekee; na


(xiii) iendelee kufuatilia taasisi na asasi zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura.

### 4.5 Wapiga Kura Wenye Mahitaji Maalum

Kwa kuzingatia maelekezo ya Tume, watu wenye mahitaji maalum kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na wenye watoto wachanga waliokuja nao vituoni walitakiwa kupewa kipaumbele siku ya kupiga kura. Tathmini ililenga kubaini iwapo maelekezo haya yalitekelezwa na kama kulikuwa na changamoto katika utekelezaji wake.

Waliohojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu watu wenye mahitaji maalum na makundi maalum katika jamii kupewa kipaumbele wakati wa kupiga kura. Wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 664 kati ya 752 waliohojiwa sawa na asilimia 88.3 walisema kuwa watu wenye mahitaji maalum na makundi maalum katika jamii walipewa kipaumbele wakati wa kupiga kura. Aidha, wahojiwa 88 sawa na asilimia 11.7 walisema kuwa makundi maalum hayakupewa kipaumbele wakati wa kupiga kura kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 4.

**Chati Na. 4: Wapiga Kura Wenye Mahitaji Maalum na Makundi Maalum katika Jamii Kupewa Kipaumbele Siku ya Kupiga Kura**




## 4.6 Ushirikishwaji wa Wadau wa Uchaguzi

Tume katika kutekeleza majukumu yake hushirikisha wadau mbalimbali ili kuweka uwazi na kupata maoni ya kuboresha mchakato wa uchaguzi. Wadau ambao hushirikishwa ni pamoja na vyama vya siasa, wapiga kura, viongozi wa dini, taasisi na asasi mbalimbali, vyombo vya habari, wazee wa kimila, makundi maalum katika jamii kama vile wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Tathmini ililenga kupata maoni kuhusu ushirikishwaji wa wadau katika zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Viongozi wa vyama vya siasa 307 walihojiwa kuhusu Tume inavyoshirikisha wadau wakati wa mchakato wa uchaguzi. Wahojiwa 261 kati ya 307 ambao ni sawa na asilimia 85 walieleza kuwa, ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi katika mchakato wa uchaguzi ulikuwa mzuri.

Aidha, viongozi wa vyama vya siasa 46 waliohojiwa sawa na asilimia 15 walieleza kuwa, ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi haukuwa mzuri. Miongoni mwa sababu zilizotolewa ni kutozingatiwa kwa mapendekezo au ushauri walioutoa kuboresha uendeshaji uchaguzi.

Matokeo haya yanaonesha kuwa, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi ulikuwa mzuri na wakuridhisha. Aidha, ili kuongeza ushiriki wa wadau wa uchaguzi katika chaguzi zijazo, mapendekezo yafuatayo yalitolewa:-

(i) Serikali iwezeshe taasisi na asasi zinazotoa elimu ya mpiga kura;

(ii) Tume iendelee kutoa elimu kwa wapiga kura kupitia njia mbalimbali kama vile vyombo vya habari, redio za kijamii na mikutano ya wadau;

(iii) machapisho mbalimbali ya elimu ya mpiga kura yatolewe ya kutosha;

(iv) sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili;

(v) uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu usimamiwe na mamlaka moja;

(vi) elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia ziwe endelevu;

(vii) wapiga kura waruhusiwe kupiga kura ya Rais katika kituo chochote;

(viii) watanzania wanaoishi nje ya nchi *(diaspora)* waruhusiwe kupiga kura;

(ix) ushiriki wa wanawake na vijana kwenye mchakato wa uchaguzi uboreshwe; na

(x) kuboresha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum kwenye mchakato wote wa uchaguzi ikiwemo kampeni.

### 4.7 Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura

Katika zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 waliajiriwa watendaji wa vituo 407,835 kwa ajili ya kusimamia na kuendesha zoezi la uchaguzi vituoni. Kati ya hao, wasimamizi wa vituo walikuwa 81,567, wasimamizi wasaidizi wa vituo 163,134 na makarani waongozaji 81,567. Aidha, kulikuwa na walinzi wa vituo 81,567 ambao walihusika na ulinzi na usalama wa vituo vya kupigia kura.

Tathmini ililenga kubaini iwapo watendaji waliokuwa katika vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi walitekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo yaliyotolewa na Tume. Aidha, ilikusudia kubaini iwapo makarani waongozaji waliweza kuwasaidia wapiga kura kujua vyumba vyao vya kupigia kura.

Matokeo haya yanaonesha kuwa, wahojiwa 572 kati ya 752 ambao ni wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa sawa na asilimia 76.1 walieleza kuwa watendaji waliokuwa katika vituo vya kupigia kura walifuata taratibu, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume.

Wahojiwa 180 sawa na asilimia 23.9 walieleza kuwa watendaji wa vituo hawakufuata sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume. Aidha, matokeo haya yanaonesha kuwa, watendaji waliokuwa katika vituo vya kupigia kura walifanya kazi zao kwa kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume hali iliyowezesha zoezi la uchaguzi kukamilika kwa amani na utulivu.

Matokeo haya vilevile yanaonesha kuwa, watu 660 kati ya 752 waliohojiwa sawa na asilimia 87.8 walisema kuwa makarani waongozaji waliwasaidia wapiga kura kutambua vyumba vya kupigia kura, wakati waliohojiwa 92 sawa na asilimia 12.2 walisema kuwa makarani waongozaji hawakuwasaidia wapiga kura kutambua vyumba vya kupigia kura. Matokeo haya yanaashiria kuwa, makarani waongozaji waliwasaidia wapiga kura kutambua vyumba wanavyopaswa kupigia kura siku ya uchaguzi.

### 4.8 Kampeni za Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 51 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 53 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, wakati wa uchaguzi wagombea hupewa fursa ya kufanya kampeni kunadi sera zao kwa wananchi. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, kampeni zilianza tarehe 26 Agosti, 2020 na kumalizika tarehe 27 Oktoba, 2020 kwa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar zilimalizika tarehe 26 Oktoba, 2020 ili kupisha kura ya mapema.

Tathmini ililenga kubaini jinsi kampeni zilivyoendeshwa na maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa. Waliohojiwa 1,706 walitoa maoni kuhusu kampeni za uchaguzi zilivyoendeshwa. Kati ya hao, 954 walikuwa watendaji wa uchaguzi na 752 wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa.

Watu 1,492 kati ya 1,706 waliohojiwa sawa na asilimia 87.5 walieleza kuwa kampeni ziliendeshwa vizuri. Aidha, waliohojiwa 81 sawa na asilimia 4.7 walieleza kuwa kampeni hazikuendeshwa vizuri na 133

ambao ni sawa na asilimia 7.8 walieleza kuwa kampeni ziliendeshwa vizuri ila zinahitaji kuboreshwa.

Matokeo yanaonesha kuwa kampeni katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ziliendeshwa vizuri na wagombea walipata fursa ya kunadi sera zao kwa wananchi ili wachaguliwe. Aidha, wakati wa majadiliano ya makundi maalum (*Focus Group Discussion - FGD*) ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake walioshiriki, walieleza kuwa kampeni zilifanyika vizuri katika maeneo yao.

Hata hivyo, baadhi ya watu waliohojiwa walipendekeza kuwa Tume iboreshe baadhi ya mambo ili kufanya uendeshaji wa kampeni kuwa bora zaidi. Mambo yaliyopendekezwa kuboreshwa ni haya yafuatayo:-

(i) kamati za maadili ya uchaguzi na kamati za uratibu wa kampeni ziwezeshwe nauli na posho za vikao zinapokutana;

(ii) wagombea wote watoe nafasi kwa wapiga kura kuuliza maswali na kutoa kero zao katika mikutano ya kampeni;

(iii) kuwe na muda maalum wa kufanya maboresho katika ratiba za kampeni za wagombea na taarifa ya mabadiliko ya ratiba za kampeni zitolewe kwa wakati;

(iv) Mwenyekiti wa kamati ya uratibu wa kampeni awe na mamlaka ya kubadili ratiba ya kampeni anapopokea maombi ya mabadiliko bila ya kusubiri vikao vya wajumbe wote;

(v) ulinzi uimarishwe katika mikutano ya kampeni;

(vi) vyama visisitizwe kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume katika kuendesha kampeni wakati wa uchaguzi; na

(vii) ruzuku itolewe kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu ili kuweka usawa kwa vyama vyote katika kuendesha kampeni.

### 4.9 Vifaa vya Uchaguzi

Tume ilifanya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na uchapishaji wa fomu, sheria za uchaguzi, kanuni na maelekezo. Vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na bahasha, mabango, shajala, wino usiofutika, taa na betri zake, vituturi, masanduku ya kura, lakiri na vifaa vya elimu ya mpiga kura na uchapishaji wa karatasi za kura na mfano wa karatasi za kura. Tume ilihakikisha kuwa, vifaa vilivyonunuliwa vinapelekwa kwa wakati katika wilaya na halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kufanikisha zoezi la uchaguzi.

Tathmini ililenga kubaini iwapo vifaa vilivyonunuliwa na kupelekwa katika maeneo ambayo uchaguzi ulifanyika vilikidhi mahitaji na vilikuwa na ubora unaotakiwa. Matokeo ya tathmini yanaonesha kuwa watendaji wa uchaguzi 926 walihojiwa, kati ya watendaji hao 940 sawa na asilimia 99.0 walieleza kuwa vifaa vilivyopelekwa katika wilaya na halmashauri vilikidhi mahitaji, wakati waliohojiwa 14 sawa na asilimia 1.0 walieleza kuwa vifaa vilivyopelekwa havikukidhi mahitaji.

Matokeo haya yanaonesha kuwa, vifaa vya uchaguzi vilivyopelekwa katika halmashauri mbalimbali nchini vilitosheleza mahitaji hali iliyowezesha uchaguzi kufanyika. Aidha, kwa maeneo machache kwa mfano halmashauri za wilaya za Songwe, Busokelo na Sumbawanga ambazo vifaa vilipelekwa pungufu Tume ilifanya jitihada za kupeleka vifaa hivyo kabla ya siku ya uchaguzi.

Kuhusu ubora wa vifaa vilivyopelekwa katika halmashauri kwa ajili ya kuendesha zoezi la uchaguzi, matokeo yanaonesha kuwa watendaji 930 kati ya 954 waliohojiwa sawa na asilimia 97 walieleza vifaa vilikuwa vina ubora unaotakiwa wakati waliohojiwa 24 sawa na asilimia 3 walieleza, vifaa havikuwa na ubora unaotakiwa.

Matokeo haya yanaonesha kuwa vifaa vya uchaguzi vilivyonunuliwa na Tume vilikuwa na ubora unaotakiwa kwa ajili ya kufanikisha zoezi la uchaguzi. Vilevile, katika kusambaza vifaa, Tume ilijitahidi kuhakikisha vifaa vyote vyenye hitilafu vinabadilishwa kabla ya siku ya uchaguzi.

Aidha, waliohojiwa walitakiwa kuainisha changamoto walizokutana nazo wakati wa kupokea, kusambaza na kuhifadhi vifaa vya uchaguzi katika maeneo yao. Zifuatazo ni baadhi ya changamoto zilizoainishwa:-

(i) baadhi ya maeneo yalikuwa hayafikiki kwa urahisi kutokana na ubovu wa miundombinu ya barabara, mfano halmashauri za wilaya za Kisarawe, Mkuranga, Malinyi, Ulanga na Gairo;

(ii) kuwepo kwa mvua wakati wa kipindi cha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iii) baadhi ya vifaa kuchelewa kufika katika baadhi ya vituo, mfano Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na halmashauri za wilaya za Kalambo, Mbeya na Gairo; na

(iv) baadhi ya maeneo kukosa sehemu salama za kuhifadhia vifaa kama vile stoo mfano Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

### 4.10 Mawakala wa Vyama vya Siasa

Kwa kuzingatia kifungu cha 57 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 58 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 vyama vya siasa viliweka mawakala katika kila kituo cha kupigia kura.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, wasimamizi wa uchaguzi waliwaapisha mawakala wa vyama vya siasa kwa vyama ambavyo viliwasilisha orodha na utambulisho wa mawakala tarehe 21 Oktoba, 2020 hadi tarehe 23 Oktoba, 2020. Hii ni baada ya Tume kuongeza siku mbili kwa ajili ya utekelezaji wa zoezi hilo. Tathmini ililenga kubaini endapo mawakala wa vyama vya siasa waliapishwa na kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati, changamoto zilizojitokeza katika utaratibu wa kuwatambulisha, kuwaapisha na utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo yaliyotolewa na Tume.

### 4.10.1 Kiapo cha Mawakala


Viongozi wa vyama vya siasa 307 walihojiwa kuhusu zoezi la kuapisha mawakala na utaratibu uliotumika kuwaruhusu kuingia katika vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi. Waliohojiwa walitoka katika baadhi ya vyama vya siasa vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Watu 257 kati ya 307 waliohojiwa ambao ni sawa na asilimia 83.7 walisema mawakala waliapishwa na kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati. Wakati waliohojiwa 38 sawa na asilimia 12.4 walisema kuwa, mawakala hawakuapishwa wala kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao kwa wakati. Aidha, waliohojiwa 12 sawa na asilimia 3.9 walisema hawajui lolote kuhusiana na suala hili.

Kwa kiasi kikubwa, matokeo yanaonesha kuwa mawakala wa vyama vya siasa waliokidhi matakwa ya kisheria na kikanuni walipata fursa ya kuapishwa na kutekeleza majukumu yao. Pia, matokeo yanaonesha kuwa, mawakala katika maeneo mengi waliapishwa kwa wakati na kuruhusiwa kutekeleza majukumu yao siku ya uchaguzi.

### 4.10.2 Mawakala Kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume

Kati ya watendaji wa uchaguzi 954 waliohojiwa, 915 sawa na asilimia 95.9 walieleza kuwa mawakala wa vyama vya siasa katika vituo vya kupigia kura walizingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo yaliyotolewa na Tume. Aidha, watendaji 39 sawa na asilimia 4.1 walisema kuwa mawakala wa vyama vya siasa hawakuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo yaliyotolewa na Tume kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 5.

**Chati Na. 5: Mawakala Kuzingatia au Kutozingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume**




Matokeo haya yanaonesha kuwa mawakala waliokuwa katika vituo vya kupigia kura walizingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya Tume hali iliyowezesha kuwa na amani na utulivu katika vituo vingi vya kupigia kura siku ya uchaguzi.

Vilevile, tathmini imebainisha changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa kuwaapisha mawakala wa vyama vya siasa na wakati wa kutekeleza majukumu yao. Changamoto hizo zilionesha kuwa baadhi ya:-

(i) vyama vya siasa kuwasilisha zaidi ya wakala mmoja kwa kituo cha kupigia kura kinyume cha sheria za uchaguzi;

(ii) vyama vya siasa vilitaka kubadili mawakala baada ya kuapishwa;

(iii) utambulisho wa mawakala katika baadhi ya maeneo ulicheleweshwa hali iliyosababisha mawakala kuchelewa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura;

(iv) wagombea kuwakataa mawakala wa vyama vyao;

(v) mawakala wa vyama vya siasa kutojua kusoma na kuandika;

(vi) mawakala wa vyama vya siasa kutaka kuingia kwenye vituo tofauti ya vituo walivyopangiwa na vyama vyao;

(vii) vyama vya siasa kuwaondoa mawakala wao katika vituo vya kupigia kura;

(viii) mawakala kutaka kuingilia majukumu ya watendaji wa vituo na baadhi yao kusababisha fujo na uharibifu wa mali; na

(ix) mawakala wa vyama vya siasa kutambulishwa na chama zaidi ya kimoja.

## 4.11 Vituo vya Kupigia Kura

Tume ilipanga vituo vya kupigia kura kwa kuzingatia idadi ya wapiga kura walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika kila kituo. Jumla ya vituo vya kupigia kura 81,567 vilipangwa kwa kuzingatia idadi ya wapiga kura wasiozidi 500 kwa kila kituo. Kati ya hivyo, vituo 80,155 vilitokana na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura walioandikishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na vituo 1,412 vilitokana na Daftari la Wapiga Kura walioandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Aidha, wasimamizi wa uchaguzi walifanya uhakiki wa vituo vya kupigia kura pamoja na ujenzi wa vituo vya


muda katika maeneo ya wazi ambayo hayakuwa na majengo ya Umma.

Tathmini ililenga kubaini endapo wapiga kura waliweza kufika katika vituo vya kupiga kura kwa urahisi na endapo mazingira ya vituo yalikuwa rafiki na salama kwa wapiga kura.

### 4.11.1 Kufikika kwa Vituo vya Kupigia Kura

Waliohojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu urahisi wa kufika au vinginevyo kwenye vituo vya kupigia kura. Watu 654 kati ya 752 waliohojiwa sawa na asilimia 86.9 walisema vituo vya kupigia kura vilifikika kwa urahisi. Wakati waliohojiwa 98 sawa na asilimia 13.1 walisema vituo vya kupigia kura havikufikika kwa urahisi. Matokeo haya ni kama yanavyooneshwa katika Chati Na. 6.

**Chati Na. 6: Kufikika kwa Vituo vya Kupigia Kura**




Matokeo haya yanaonesha kuwa vituo vya kupigia kura katika maeneo mengi nchini vilifikika kwa urahisi.

### 4.11.2 Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura

Waliohojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu usalama wa vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi. Matokeo yanaonesha kuwa waliohojiwa 687, kati ya 752 sawa na asilimia 91.4 walisema vituo vya kupigia kura vilikuwa katika mazingira rafiki na salama kwa wapiga kura wakati wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa 65 waliohojiwa sawa na asilimia 8.6 walisema vituo havikuwa mazingira rafiki na salama kwa ajili ya kupigia kura.

Aidha, tathmini imebaini kuwa, katika maeneo machache kulikuwa na changamoto ya vituo vya wazi kukosa huduma ya vyoo, ubora unaohitajika, kuwa katika vyumba vidogo na kukosekana kwa ulinzi wa kutosha katika baadhi ya vituo vya kupigia kura. Matokeo haya ni kama yanavyooneshwa kwenye Chati Na. 7.

**Chati Na. 7: Usalama wa Vituo vya Kupigia Kura**




Matokeo haya yanaonesha kuwa vituo vya kupigia kura katika maeneo mengi vilikuwa katika mazingira rafiki na salama kwa ajili ya kupiga kura.

## 4.12 Kupiga na Kuhesabu Kura

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 jumla ya wapiga kura 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 walijitokeza kupiga kura za Rais na Makamu wa Rais kati ya wapiga kura 29,754,696 ya walioandikishwa. Kati ya kura zilizopigwa kura halali zilikuwa 14,830,195 sawa na asilimia 98. 3 ya kura zote zilizopigwa. Idadi ya kura zilizokataliwa zilikuwa 261,755 sawa na asilimia 1.7 ya kura zote 15,091,950 zilizopigwa ikiwa ni zaidi ya lengo la Tume kuhakikisha kuwa, kura zinazokataliwa hazizidi asilimia 1.6.


Tathmini ililenga kubaini endapo vituo vya kupigia kura vilifunguliwa kwa wakati siku ya uchaguzi. Vilevile, ilikusudiwa

kubaini umri na jinsi ya wapiga kura waliojitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi na changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la kupiga na kuhesabu kura.

### 4.12.1 Muda wa Kufungua Vituo vya Kupigia Kura

Jumla ya wahojiwa 752 kutoka katika kundi la wapiga kura na viongozi wa vyama vya siasa waliulizwa kuhusu muda ambao vituo vilifunguliwa siku ya kupiga kura. Watu 710 kati ya 752 waliohojiwa sawa na asilimia 94.4 walieleza kuwa vituo vilifunguliwa kwa wakati, ambapo 26 sawa na asilimia 3.5 ya waliohojiwa walieleza kuwa vituo havikufunguliwa kwa wakati na watu 16 sawa na asilimia 2.1 ya waliohojiwa walieleza kuwa hawajui. Matokeo haya yanaoneshwa katika Chati Na. 8.

**Chati Na. 8: Muda wa Kufungua Vituo vya Kupigia Kura**



Matokeo yanaonesha kuwa vituo vya kupigia kura katika maeneo mengi vilifunguliwa kwa wakati uliopangwa kama ilivyoelekezwa na Tume. Hata hivyo, baadhi ya wadau waliishauri Tume kuzingatia muda wa kufungua vituo kwa kuwa katika maeneo yao vituo vilichelewa kufunguliwa.

### 4.12.2 Jinsi ya Wapiga Kura


Tathmini ililenga kubaini jinsi ya wapiga kura waliojitokeza kupiga kura siku ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Kati ya wapiga kura 445 waliohojiwa ni wapiga kura 441 ndio waliojitokeza kwenda kupiga kura.

Matokeo yanaonesha kuwa, wapiga kura 290 kati ya 441 waliojitokeza kupiga kura sawa na asilimia 65.8 walikuwa wanawake na wapiga kura 151 sawa na asilimia 34.2 walikuwa wanaume. Matokeo haya yanaonesha kuwa wanawake katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 walijitokeza kwa wingi kupiga kura ikilinganishwa na wanaume.

### 4.12.3 Umri wa Wapiga Kura Waliojitokeza Kupiga Kura

Wapiga kura 445 waliulizwa kuhusu kujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi. Wapiga kura 441 kati ya 445 ya waliohojiwa sawa na asilimia 99.1 walieleza kuwa, walijitokeza kupiga kura, wahojiwa 4 sawa na asilimia 0.9 walisema hawakujitokeza kupiga kura. Kuhusu umri wa wapiga kura waliojitokeza siku ya kupiga kura, wahojiwa 98 kati ya 441 sawa na asilimia 22.3 walikuwa vijana (umri kati ya miaka 18 – 35), wahojiwa 288 sawa na asilimia 65.3 walikuwa watu wa makamo (umri kati ya miaka 36 – 64) wakati wahojiwa 55 sawa na asilimia 12.4 walikuwa wazee (umri wa miaka 65 na zaidi) kama inavyooneshwa kwenye Chati Na. 9.

**Chati Na. 9: Makundi kwa Umri wa Wapiga Kura Waliojitokeza Kupiga Kura**




Matokeo haya yanaonesha kuwa, watu wa makamo katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 walijitokeza kwa wingi ikilinganishwa na makundi mengine.

### 4.12.4 Changamoto Wakati wa Kupiga na Kuhesabu Kura

Watendaji wa uchaguzi 954 waliulizwa kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa changamoto wakati wa kupiga na kuhesabu kura. Waliohojiwa 784 kati ya 954 sawa na asilimia 82.2 walieleza kuwa hakukuwa na changamoto zozote katika zoezi la kupiga kura wakati watendaji 170 sawa na asilimia 17.8 ya waliohojiwa walieleza kulikuwa na changamoto. Matokeo haya ni kama inavyooneshwa katika Chati Na. 10.

**Chati Na. 10: Changamoto Wakati wa Kupiga na Kuhesabu Kura**




Matokeo yanaonesha kuwa, zoezi la kupiga na kuhesabu kura katika maeneo mengi lilifanyika vizuri. Hali hiyo ilitoa fursa kwa wapiga

kura kuwachagua wagombea waliowataka. Wakati wa majadiliano na makundi maalum ya wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na vijana walieleza kuwa, katika maeneo wanayotoka zoezi la kupiga na kuhesabu kura liliendeshwa kwa amani na utulivu.

Vilevile, walielezea kuridhishwa na utendaji wa watendaji wa vituo siku ya uchaguzi na suala la upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wote wa uchaguzi. Baadhi ya waliohojiwa walitoa maoni kuwa zoezi la kupiga kura lianze saa kumi na mbili (12:00) asubuhi badala ya saa moja (1:00) asubuhi ili kuwapa fursa wapiga kura wenye majukumu mengine kuwahi kupiga kura.

### 4.12.5 Kura Zilizokataliwa

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Tume iliweka lengo la kupuguza kura zitakazokataliwa kutoka asilimia 2.58 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 1.6 ya kura zote zitakazopigwa. Hata hivyo, hali halisi imeonesha kura zilizokataliwa katika uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ni asilimia 1.73 ambayo ni zaidi ya lengo lililowekwa. Watendaji wa uchaguzi walihojiwa ili kubaini sababu za ongezeko la idadi ya kura zilizokataliwa. Sababu zilizobainishwa ni pamoja na:-

(i) elimu ya mpiga kura kutofikia wapiga kura wengi katika baadhi ya maeneo;

(ii) kutojua kusoma na kuandika; na

(iii) baadhi ya wapiga kura kuharibu kura kwa makusudi.

### 4.13 Kuhesabu, Kujumlisha na Kutangaza Matokeo

Mara baada ya kukamilika kwa zoezi la kupiga kura, vituo vya kupigia kura vilitumika kwa ajili ya zoezi la kuhesabu kura. Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura walihesabu kura huku wakishuhudiwa na watu wanaoruhusiwa kisheria kuwepo wakati wa kuhesabu kura ikiwemo mawakala wa vyama vya siasa.

Kabla ya kuanza kuhesabu kura masanduku ya kura yalikaguliwa ili kuthibitisha kuwa lakiri hazijafunguliwa. Hatua hiyo ilifuatiwa na wasimamizi wa vituo kufungua sanduku moja baada ya lingine na kuhesabu kura zote zilizomo ndani ya sanduku, kura alizopata kila mgombea na kura zilizokataliwa au kuharibika. Utaratibu wa kuhesabu kura ulizingatia misingi ya uwazi na mawakala walijaza Fomu Na. 16 kuonesha kuridhika au kutoridhika katika kila hatua ya kuhesabu kura.

Wasimamizi wa vituo baada ya kuhesabu kura walijaza fomu za matokeo, Fomu Na. 21A kwa matokeo ya kiti cha Rais, Fomu Na. 21B kwa matokeo ya Ubunge na Fomu Na. 21C kwa matokeo ya Udiwani ambazo zilisainiwa na mawakala. Aidha, Wasimamizi wa vituo walibandika nakala za matokeo haya nje ya kituo cha kupigia kura na nakala nyingine waliwapatia mawakala. Baada ya kukamilika kwa mchakato wa kuhesabu kura vituoni fomu za matokeo na vifaa vilipelekwa kwa wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata kwa ajili ya majumuisho ya kura.

Msimamizi wa uchaguzi baada ya kujumlisha kura za Mbunge alimtangaza mgombea aliyeshinda na kubandika matokeo nje ya kituo cha kujumlishia matokeo. Msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata baada ya kujumlisha kura za Udiwani alimtangaza mgombea aliyeshinda na kubandika matokeo nje ya kituo cha majumuisho. Tathmini ililenga kubaini endapo kulikuwa na changamoto katika hatua ya kujumlisha na kutangaza matokeo ngazi ya kata na jimbo.

#### 4.13.1 Matokeo ya Tathmini Kuhesabu, Kujumlisha na Kutangaza Matokeo


Watendaji wa uchaguzi 954 waliulizwa kuhusu changamoto wakati wa mchakato wa kujumlisha kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi. Watendaji 870 waliohojiwa kati ya 954 sawa na asilimia 91.2 walieleza kuwa hakukuwa na changamoto, wakati watendaji 84 sawa na asilimia 8.8 walitoa taarifa kuwa kulikuwa na changamoto ambazo Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuzifanyia kazi.

Matokeo haya yanaonesha kuwa zoezi la kujumlisha na kutangaza matokeo katika maeneo mengi lilifanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo ya Tume hali iliyowezesha wagombea walioshinda kutangazwa kuwa washindi. Katika majadiliano na makundi ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake walieleza kuwa mchakato wa utangazaji wa matokeo ulienda vizuri katika maeneo yao na matokeo yalitangazwa kwa wakati.

Pia, tathmini ililenga kubaini endapo kulikuwa na changamoto katika kutuma matokeo ya kiti cha Rais kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Waliohojiwa 874 sawa na asilimia 92.0 walieleza kuwa hakukuwa na

changamoto yoyote katika utumaji wa matokeo kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati waliohojiwa 80 sawa na asilimia 8.0 walieleza kuwa kulikuwa na changamoto katika utumaji wa matokeo kwenda Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Changamoto hizo ni pamoja na kukosekana kwa huduma ya mtandao wa *internet* na tatizo la umeme katika baadhi ya maeneo. Matokeo haya yameoneshwa katika Chati Na. 11.

**Chati Na. 11: Utumaji wa Matokeo ya Kiti cha Rais kwenda Tume**




Matokeo yanaonesha kuwa, katika maeneo mengi, zoezi la kutuma matokeo lilifanyika vizuri bila kuwa na changamoto hali ambayo iliiwezesha Tume kumtangaza mshindi wa kiti cha Rais ndani ya saa 48.


Hata hivyo, Tume haina budi kuendelea kuzifanyia kazi changamoto zilizobainishwa ikiwemo kukosekana kwa huduma za mawasiliano

katika baadhi ya halmashauri, matatizo ya mtandao wa *internet* kwa baadhi ya maeneo na tatizo la umeme.

### 4.14 Mwitikio wa Wapiga Kura

Idadi ya wapiga kura waliojitokeza kupiga kura ya kiti cha Rais katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ni 15,091,950 sawa na asilimia 50.72 ya wapiga kura 29,754,696 walioandikishwa. Mwitikio huu ni mdogo ikilinganishwa na asilimia 67.34 ya wapiga kura 15,596,110 waliojitokeza kupiga kura ya kiti cha Rais kati ya wapiga kura ya 23,161,440 waliojiandikisha katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Chati Na. 12 inaonesha mwitikio wa wapiga kura katika chaguzi kuu sita (6) zilizopita.

**Chati Na. 12: Mwitikio wa Wapiga Kura kwa Chaguzi Kuu Sita**




Tathmini ililenga kubaini mambo yaliyosababisha asilimia ya wapiga kura waliojitokeza kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka

2020 kupungua na kupata maoni ya nini kifanyike ili kuongeza idadi ya wapiga kura wanaojitokeza kupiga kura katika chaguzi zijazo.

Katika tathmini ya mwitikio wa wapiga kura, jumla ya mikutano na mijadala 24 ilifanyika. Walengwa wa mikutano hiyo walitoka kwenye makundi mbalimbali wakiwemo makundi ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake.

Waliohojiwa waliulizwa kuhusu mwitikio mdogo wa wapiga kura kwa baadhi ya maeneo siku ya kupiga kura. Baadhi ya sababu zilizobainishwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) baadhi ya wapiga kura kuwa maeneo tofauti na vilipo vituo walivyojiandikishia siku ya kupiga kura kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kazi, kilimo, safari na masomo;
(ii) elimu ya mpiga kura iliyotolewa kutofika katika baadhi ya maeneo;
(iii) kukosekana kwa elimu ya uraia ya kutosha;
(iv) umbali wa vituo vya kupigia kura kwa baadhi ya maeneo;
(v) baadhi ya wagombea kushindwa kutekeleza ahadi wanazotoa wakati wa kampeni;
(vi) wagombea kuchaguliwa bila kupingwa katika baadhi ya maeneo;
(vii) baadhi ya wapiga kura kupoteza kadi za kupigia kura;
(viii) hofu ya usalama wakati wa kupiga kura kwa baadhi ya maeneo;
(ix) baadhi ya wapiga kura kuwa na imani kuwa mgombea wa chama fulani atashinda;
(x) wapiga kura kujikita zaidi katika shughuli nyingine za uzalishaji siku ya kupiga kura;

(xi) baadhi ya vyama kuwashawishi wapiga kura wasiende kupiga kura;
(xii) baadhi ya vyama kukosa sera bora za kuwavutia wapiga kura;
(xiii) hali ya hewa katika baadhi ya maeneo hususan maeneo yenye mvua kipindi cha mwezi Oktoba;
(xiv) baadhi ya wananchi kujiandikisha kupiga kura kwa lengo la kupata kadi ya mpiga kura ili waitumie kwa shughuli nyingine;
(xv) baadhi ya wapiga kura kutohakiki majina yao kwenye Daftari hivyo kushindwa kufahamu vituo watakavyopigia kura vilipo;
(xvi) baadhi ya vyama kushindwa kufanya kampeni za kutosha katika maeneo yote; na
(xvii) baadhi ya vyama kununua kadi za wapiga kura ili wapiga kura washindwe kwenda kupiga kura.

Walengwa wa zoezi la tathmini kutoka katika makundi ya wazee, vijana, watu wenye ulemavu na wanawake walipendekeza mambo yafuatayo ili kuboresha mwitikio wa wapiga kura katika chaguzi zijazo. Baadhi ya mambo yaliyopendekezwa ni yafuatayo:-

(i) elimu ya mpiga kura iwe endelevu;
(ii) taasisi na asasi zinazohusika na utoaji wa elimu ya mpiga kura ziruhusiwe kutoa elimu endelevu;
(iii) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uwe endelevu;
(iv) watendaji wa Tume waendelee kusimamia uchaguzi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya kazi bila upendeleo; na

(v) Tume ianzishe utaratibu wa kupiga kura kwa njia ya mtandao (*electronic voting*).

## 4.15 Taarifa za Watazamaji wa Uchaguzi, Taasisi na Asasi zilizotoa Elimu ya Mpiga Kura

Kwa kuzingatia kanuni ya 23(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, watazamaji wa uchaguzi wanatakiwa, katika kipindi kisichozidi miezi miwili tangu tarehe ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi kuwasilisha taarifa zao Tume.

Jumla ya taasisi na asasi 18 kati ya taasisi na asasi 117 zilizopewa vibali vya kutazama uchaguzi mkuu zilitekeleza takwa hilo la kisheria. Kati ya taasisi na asasi 18 zilizowasilisha taarifa za utazamaji wa uchaguzi, 13 ni za ndani ya nchi wakati 5 ni taasisi za kimataifa. Maoni na mapendekezo mbalimbali yalitolewa katika taarifa za watazamaji zilizowasilishwa.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 4C cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ilitoa vibali kwa asasi 252 kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo mbalimbali wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Taasisi na asasi 107 ndizo zilizowasilisha taarifa zao kuhusu namna walivyotoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mkuu.

Aidha, watazamaji wa uchaguzi, taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura walionesha kuridhishwa na jinsi zoezi la uchaguzi

liivyoendeshwa na kuainisha mafanikio, changamoto, maoni na mapendekezo kwa Tume.

### 4.15.1 Mafanikio

Tume baada ya kupokea taarifa za watazamaji, taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura, ilipitia taarifa hizo ambazo pamoja na mambo mengine, ziliainisha mafanikio katika mambo yafuatayo:-

(i) kuendesha uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika;

(ii) kuwepo idadi kubwa ya vituo vya kupigia kura na vinavyofikika;

(iii) kutangaza matokeo ndani ya saa 48 baada ya zoezi la kupiga kura kukamilika;

(iv) wapiga kura kutumia muda mfupi katika vituo vya kupigia kura ambao ni wastani wa dakika 6 kupiga kura;

(v) kuendelea kuweka majalada ya nukta nundu (Tactile ballot folder) katika vituo vya kupigia kura kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu wa kutokuona kupiga kura;

(vi) muda wa kutosha uliotolewa kwa wagombea kufanya kampeni na kampeni kufanyika kwa amani na utulivu;

(vii) kuwepo kwa amani na utulivu siku ya kupiga kura;

(viii) kuwepo kwa mawakala wa vyama vya siasa katika vituo vya kupigia kura;

(ix) wapiga kura wenye mahitaji maalum kusaidiwa bila kubughudhiwa vituoni;

(x) vituo vingi kufunguliwa na kufungwa kwa wakati kama ilivyoelekezwa katika sheria;

(xi) kuwepo kwa vifaa vya kupigia kura katika vituo vyote vya kupigia kura; na

(xii) uchaguzi kufanyika siku ya Jumatano na Serikali kuitangaza siku hiyo kuwa siku ya mapumziko.

### 4.15.2 Changamoto

Tume baada ya kupokea taarifa za watazamaji na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura, ilipitia taarifa hizo ambazo pamoja na mambo mengine ziliainisha changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) baadhi ya vituo kuwa katika vyumba vidogo;

(ii) baadhi ya vifaa kuchelewa kufika katika baadhi ya vituo;

(iii) baadhi ya wapiga kura kutokuwa katika maeneo waliojiandikisha hivyo kushindwa kupiga kura;

(iv) baadhi ya taasisi na asasi kukosa fedha kwa ajili ya kuendesha elimu ya mpiga kura; na

(v) elimu ya mpiga kura kutopewa muda wa kutosha hali iliyosababisha kiwango kidogo cha wapiga kura waliojitokeza siku ya uchaguzi Mkuu.

### 4.15.3 Maoni na Mapendekezo

Mikutano mbalimbali ya wadau iliyofanyika nchi nzima kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uchaguzi mkuu ulivyoendeshwa.

Maoni na mapendekezo mbalimbali ya kuboresha chaguzi zijazo yalitolewa kama yafuatayo:-

(i) sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili;

(ii) uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu zisimamiwe na mamlaka moja;

(iii) elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia iwe endelevu;

(iv) Serikali iwezeshe taasisi na asasi zinazotoa elimu ya mpiga kura;

(v) wapiga kura waruhusiwe kupiga kura ya Rais katika kituo chochote;

(vi) watanzania wanaoishi nje ya nchi *(diaspora)* waruhusiwe kupiga kura;

(vii) wagombea Ubunge na Udiwani wanaochaguliwa bila kupingwa wapigiwe kura;

(viii) ushiriki wa wanawake na vijana kwenye mchakato wa uchaguzi uboreshwe;

(ix) kuboresha ushiriki wa watu wenye mahitaji maalum kwenye mchakato wote wa uchaguzi ikiwemo kampeni;

(x) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uwe endelevu;

(xi) kuunganisha mifumo ya usajili na utambuzi wa watu ili kurahisisha zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(xii) vituo vya kupigia kura viongezwe katika baadhi ya maeneo ili kuwa karibu zaidi na wapiga kura;

(xiii) wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo na kata wapewe mamlaka ya kuapisha mawakala;

(xiv) viwango vya malipo ya watendaji wa uchaguzi viongezwe ili kuendana na mahitaji halisi;

(xv) Tume iangalie uwezekano wa kuwa na maghala au stoo zake za kuhifadhia vifaa vya uchaguzi katika halmashauri;

(xvi) maafisa TEHAMA watambuliwe kama watendaji wa uchaguzi wanaoteuliwa;

(xvii) mifumo ya TEHAMA ya uchaguzi iboreshwe zaidi kwa chaguzi zijazo;

(xviii) Tume iwe na ofisi na watendaji wake katika ngazi ya halmashauri;

(xix) Tume iangalie uwezekano wa kupiga kura kwa njia ya mtandao;

(xx) baadhi ya makundi kama polisi na watendaji wa uchaguzi watengewe siku maalum ya kupiga kura;

(xxi) kampeni ziwe na wakalimani wa lugha za alama;

(xxii) wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata wawe na mfumo wa TEHAMA wa kukusanya matokeo na kuyapeleka jimboni;

(xxiii) elimu ya uraia itiliwe mkazo zaidi;

(xxiv) mikutano ya Tume na wadau iwe endelevu;

(xxv) kuwapatia ulinzi baadhi ya watendaji wa uchaguzi ngazi ya halmashauri pamoja na familia zao wakati wa uchaguzi;

(xxvi) Tume iendelee kushirikiana na wadau wote wa uchaguzi ikiwa ni pamoja ya vyama vyote vya siasa; na

(xxvii) Tume iendelee kuwaruhusu wapiga kura ambao wamepoteza au kadi zao kuharibika ili kutumia vitambulisho mbadala kupigia kura ikiwa ni pamoja na barua za utambulisho kutoka kwa watendaji.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Hitimisho

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya Tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ikiwa ni mara ya pili tangu kuanzishwa kwake. Tathmini ya kwanza ilifanyika baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015. Kama ilivyokuwa kwa Tathmini ya mwaka 2015, tathmini hii imefanyika kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali. Wadau hao ni watendaji wa uchaguzi ambao ni (waratibu wa uchaguzi wa mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo yote, maafisa uchaguzi na maafisa ugavi kutoka Tanzania Bara), vyama vya siasa, wapiga kura, makundi maalum ya wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu, taasisi na asasi zilizotoa elimu ya mpiga kura, na watazamaji wa ndani na wa kimataifa.

Lengo la tathmini lilikuwa ni kupata maoni kutoka kwa wadau wa uchaguzi kuhusu zoezi la Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2020 lilivyoendeshwa. Pia, Tume ilitaka kupata maoni kuhusu mambo mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa sheria za uchaguzi, kanuni, maadili ya uchaguzi, miongozo na maelekezo ya Tume yalivyofanya kazi katika kusaidia kuendesha zoezi la uchaguzi.

Maeneo mengine ambayo Tume ilitaka kupata maoni ni katika utoaji wa elimu ya mpiga kura, uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, vifaa vya uchaguzi, ushirikishwaji wa wadau,ushirikishwaji wa taasisi na asasi mbalimbali, uendeshaji wa kampeni za uchaguzi, hali

ya vituo vya kupigia kura, zoezi kupiga kura lilivyofanyika, mwitikio wa wapiga kura na uwepo wa kura zilizoharibika.

Tathmini hii pia ilihusisha mapitio ya taarifa mbalimbali za watazamaji wa uchaguzi ambazo zimebainisha kuwa, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ulikuwa huru, wa haki na wa kuaminika. Vilevile, matokeo ya tathmini yameonesha kuwa katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi zilizingatiwa na wadau walipata fursa ya kushiriki kikamilifu katika mchakato wote. Aidha, matokeo yameonesha kuwa uteuzi wa wagombea, kampeni, kupiga kura na kuhesabu kura, kujumlisha na kutangaza matokeo yaliendeshwa kwa mujibu wa katiba, sheria, kanuni na maelekezo ya Tume, 2020.

Katika Tathmini iliyofanyika, Tume imebainisha changamoto zifuatazo:-

(i) baadhi ya maeneo kuwa na mwitikio mdogo wa wapiga kura uliosababishwa na baadhi ya wapiga kura kutofikiwa na elimu ya mpiga kura na uraia, kuhama makazi, umbali wa vituo, wagombea kupita bila kupingwa, hofu ya kujitokeza kwa vurugu na vitisho pamoja na uwepo wa mvua siku ya uchaguzi katika baadhi ya maeneo;

(ii) baadhi ya watu walishindwa kuboresha taarifa zao kutokana na siku zilizotengwa kwa ajili ya zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kuwa chache;

(iii) uwepo wa mvua nyingi zilizoharibu miundombinu ya barabara, hivyo kuathiri usafirishaji na usambazaji wa vifaa

vya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika baadhi ya maeneo; na

(iv) mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 wakati wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura awamu ya pili;

(v) baadhi ya asasi na taasisi zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpiga kura kushindwa kutoa elimu hiyo;

(vi) baadhi ya wananchi kushindwa kuhakiki taarifa zao hivyo kushindwa kutambua vituo vyao vya kupigia kura;

(vii) madai ya baadhi ya wagombea kuwa hawakupata majibu ya rufaa zao, wakati hakuna kumbukumbu za rufaa hizo kupokelewa wala kusajiliwa na Tume;

(viii) madai ya baadhi ya mawakala wa vyama vya siasa kuzuiliwa kuingia kwenye vituo vya kupigia kura; na

(ix) baadhi ya maeneo kampeni kutokufanyika vizuri kwa sababu baadhi ya wagombea walikiuka maadili ya uchaguzi ikiwemo kutoa lugha ya matusi, wagombea kutofanya kampeni za kutosha, hofu ya fujo jambo lililosababisha wapiga kura kutojitokeza kusikiliza sera za wagombea.

## 5.2 Mapendekezo

Tathmini ililenga pamoja na mambo mengine, kuboresha utendaji kazi wa Tume na kuongeza mwitikio wa wapiga kura katika chaguzi zijazo. Ili kufikia lengo hili, yafuatayo yanapendekezwa: -

(i) kuwe na watendaji wa Tume hadi ngazi ya halmashauri;

(ii) mamlaka husika ziangalie uwezekano wa kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo;

(iii) sheria za uchaguzi zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili;

(iv) Serikali iangalie uwezekano wa kuziwezesha kifedha asasi na taasisi zinazotoa elimu ya mpiga kura katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi;

(v) uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura uwe endelevu;

(vi) elimu ya mpiga kura iwe endelevu, msisitizo utolewe kwa matumizi ya njia zitakazowezesha Tume kuwafikia wapiga kura wengi zaidi kama vile matumizi ya redio za kijamii na elimu ya nyumba kwa nyumba kupitia viongozi wa serikali za mitaa;

(vii) elimu ya uraia itiliwe mkazo zaidi kuwafanya wananchi watambue haki yao ya kupiga kura;

(viii) utaratibu uliotumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 katika kuhesabu, kujumlisha na kutangaza matokeo na kuiwezesha Tume kutangaza matokeo hayo katika kipindi kifupi uendelezwe na ikiwezekana uboreshwe zaidi; na

(ix) sifa za wagombea Ubunge na Udiwani ziangaliwe upya hasa kipengele cha elimu kwa kuongeza sifa ya kuwa na elimu ya angalau kidato cha nne.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho Na. 1: Orodha ya Mikoa na Halmashauri/Wilaya zilizofanyiwa Tathmini**

| NA. | MIKOA | HALMASHAURI/ WILAYA | JIMBO | KATA/ SHEHIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | Arusha CC | Arusha Mjini | Sekei |
| | | | | Lemara |
| | | Arusha DC | Arumeru Magharibi | Sokoni II |
| | | | | Kiutu |
| 2. | Kilimanjaro | Moshi MC | Moshi Mjini | Kilimanjaro |
| | | | | Korongoni |
| | | | | Kiusa |
| | | | | Msaranga |
| | | Hai DC | Hai | Muungano |
| | | | | Bomang'ombe |
| | | | | Masama Kusini |
| | | | | Bondeni |
| 3. | Tanga | Korogwe TC | Korogwe Mjini | Kilole |
| | | | | Mtonga |
| | | Korogwe DC | Korogwe Vijijini | Hale |
| | | | | Mnyuzi |
| 4. | Dar es Salaam | Temeke MC | Temeke | Miburani |
| | | | | Kurasini |
| | | Ubungo MC | Ubungo | Ubungo |
| | | | | Manzese |
| 5. | Morogoro | Morogoro MC | Morogoro Mjini | Mbuyuni |
| | | | | Mji Mkuu |
| | | Mvomero DC | Movomero | Lubungo |
| | | | | Melela |
| 6. | Pwani | Kibaha TC | Kibaha Mjini | Tangini |
| | | | | Maili Moja |
| | | Kibaha DC | Kibaha Vijijini | Janga |
| | | | | Mtongani |
| 7. | Dodoma | Dodoma CC | Dodoma Mjini | Miyuji |
| | | | | Madukani |
| | | Bahi DC | Bahi | Bahi |
| | | | | Kigwe |
| 8. | Simiyu | Bariadi DC | Bariadi | Ng'uliyati |
| | | | | Dutwe |
| | | Itilima DC | Itilima | Lagangabilili |
| | | | | Budalabujiga |
| 9. | Singida | Singida MC | Singida Mjini | Kindai |

| NA. | MIKOA | HALMASHAURI/ WILAYA | JIMBO | KATA/ SHEHIA |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Mindunduruni |
| | | Ikungi DC | Singida Mashariki | Ntuntu |
| | | | | Unyahati |
| 10. | Shinyanga | Shinyanga MC | Shinyanga Mjini | Ibinzamata |
| | | | | Mjini |
| | | Kahama MC | Kahama Mjini | Kagongwa |
| | | | | Kahama Mjini |
| 11.. | Lindi | Lindi MC | Lindi Mjini | Matopeni |
| | | | | Makonde |
| | | Mtama DC | Mtama | Majengo |
| | | | | Mtama |
| 12. | Mtwara | Mtwara MC | Mtwara Mjini | Majengo |
| | | | | Vigaeni |
| | | Mtwara DC | Mtwara Vijijini | Nalingu |
| | | | | Libebe |
| 13. | Ruvuma | Songea DC | Peramiho | Peramiho |
| | | | | Litisha |
| | | Songea MC | Songea Mjini | Mfaranyaki |
| | | | | Lizabon |
| 14. | Iringa | Iringa MC | Iringa Mjini | Isakalilo |
| | | | | Kwakilosa |
| | | Kilolo DC | Kilolo | Mtitu |
| | | | | Ihimbo |
| 15. | Mbeya | Mbeya CC | Mbeya Mjini | Ilomba |
| | | | | Sisimba |
| | | Mbeya DC | mbeya Vijijini | Utenguleusomgwe |
| | | | | Msalala |
| 16. | Njombe | Makambako TC | Makambako | Maguvani |
| | | | | Mlowa |
| | | Njombe TC | Njombe Mjini | Njombe Mjini |
| | | | | Mji Mwema |
| 17. | Rukwa | Sumbawanga MC | Sumbawanga Mjini | Sumbawanga |
| | | | | Lwiche |
| | | Kalambo DC | Kalambo | Lyowa |
| | | | | Matai |
| 18. | Songwe | Tunduma TC | Tunduma | Chapwa |
| | | | | Katete |
| | | Mbozi DC | Vwawa | Ihanda |
| | | | | Ilolo |

| NA. | MIKOA | HALMASHAURI/ WILAYA | JIMBO | KATA/ SHEHIA |
|---|---|---|---|---|
| 19. | Geita | Geita TC | Geita Mjini | Kalangalala |
| | | | | Bombambili |
| | | Geita DC | Geita Vijijini | Nzera |
| | | | | Nkome |
| 20. | Mwanza | Ilemela MC | Ilemela | Kiseke |
| | | | | Kirumba |
| | | Mwanza CC | Nyamagana | Mabatini |
| | | | | Nyamagana |
| 21. | Kigoma | Kigoma MC | Kigoma Mjini | Rubuga |
| | | | | Machinjioni |
| | | Kigoma DC | Kigoma Kaskazini | Mwandiga |
| | | | | Bitale |
| 22. | Tabora | Nzega TC | Nzega Mjini | Miguwa |
| | | | | Itilo |
| | | Tabora MC | Tabora Mjini | Ipuli |
| | | | | Ng'imbo |
| 23. | Kusini Pemba | Chakechake | Chakechake | Madungu |
| | | | | Msingini |
| | | | Chonga | Kilindi |
| | | | | Matale |
| | | | | Chonga |
| 24. | Mjini Magharibi | Mjini | Kwahani | Sebleni |
| | | | | Muungano |
| | | Magharibi B | Dimani | Tomondo |
| | | | | Kisauni |

**Kiambatisho Na. 2: Mpango wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tathmini ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020**

| NA. | MAPENDEKEZO | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | VIASHIRIA VYA UPIMAJI | MUDA WA UTEKELEZAJI | RASILI MALI | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Maboresho ya Sheria za uchaguzi | a) Sheria za uchaguzi zitafasiriwe kwa lugha ya Kiswahili ili zieleweke kwa wananchi.<br>b) Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ziunganishwe pamoja ili kuondoa mkanganyiko.<br>c) Tume ifanye maboresho ya sheria ili kuhusisha maoni ya wadau | a) Kupungua kwa malalamiko kuhusu tafsiri ya sheria za uchaguzi.<br>b) Kuwepo kwa sheria moja inayojumuisha masuala yote ya uchaguzi | Mwaka 2021 - 2024 | | Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 2. | Mwitikio wa wapiga kura | a) Elimu ya mpiga kura iwe endelevu na itolewe mpaka ngazi ya kata na kijiji.<br>b) Asasi zinazotoa elimu ya mpiga kura ziwezeshwe ili ziweze kufika maeneo yasiyofikika<br>c) Elimu ya Uraia itolewe kwa ufanisi na mamlaka husika | Ongezeko la Wapiga Kura. | Mwaka 2021 - 2025 | | Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya siasa Nchini |
| 3. | Kuboresha Utoaji wa elimu ya mpiga kura | a) Tume itoe elimu endelevu ya mpiga kura katika ngazi ya kata na kijiji.<br>b) Tume iwe na vipindi maalumu vya redio na runinga mara baada ya uchaguzi mkuu ili kutoa elimu endelevu kwa wapiga kura.<br>c) Kuandaa vipeperushi pamoja na kubandika stika zenye ujumbe kuhusu elimu ya mpiga kura katika vyombo mbalimbali vya usafiri.<br>d) Kuhuisha Mpango mkakati wa elimu ya | Ongezeko la mwitikio wa wapiga kura | Mwaka 2021 - 2025 | | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |

| NA. | MAPENDEKEZO | MKAKATI WA UTEKELEZAJI | VIASHIRIA VYA UPIMAJI | MUDA WA UTEKELEZAJI | RASILI MALI | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mpiga kura ili kuweka maoni ya Wadau<br>e) Tume iwatumie viongozi wa Serikali ya mtaa/ vijiji katika kutoa elimu ya mpiga kura | | | | |
| 4. | Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la mpiga kura | a) Sheria za Uchaguzi ziboreshwe ili uboreshaji ufanyike mara kwa mara badala ya mara mbili kati ya uchaguzi mkuu mmoja na mwingine<br>b) Kuwe na ofisi za kudumu za Tume katika kila halmashauri zitakazo kuwa zinafanya uboreshaji wa mara kwa mara. | Kuongezeka kwa idadi ya wapiga kura kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. | Mwaka 2021 - 2025 | | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| 5. | Uendeshaji wa kampeni | Maadili ya uchaguzi yafanyiwe mapitio kwa lengo la kuongeza adhabu kwa wanaokiuka maadili wakati wa kampeni. | Kupungua kwa vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi. | Kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. | | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |